

MAKONGAMANO



Kisha kusikiliza shuhuda zenu, na kuingia baada ya kuwa hudumani, na kumsikia mtu fulani akishuhudia. Hakika nina furaha kumwona Ndugu Jeffries. Mimi humwita Creechy, pale. Sikujua alikuwa mkutanoni. Nami najua hili linamaanisha mengi kwenu, pia, tangu kuja kutoka kwenye uwanja wa vita, ambako nuru ni duni; na kuingia chini ya mazingira haya mazuri ya Wakristo na watu kwa jumla, huru katika Roho. Na—napenda hili, ambapo watu ni huru, wanajisikia huru. Na ni jambo fulani kulihusu. Hatujaribu tu kujifanya wagumu. Hao ni—ni ninii tu. . . Walizoea kusema, vua ukosi wako na ujisikie nyumbani. Ninapenda hilo. Nina hakika sote tunalipenda. Sivyoy?

² Ninii tu. . . Nilikuwa nikiwazia, nilipoangalia hapa kwa binti yangu, Rebekah. Nakumbuka wakati mmoja, nikiwa mbali mkutanoni. Naye alikuwa ni jamaa mdogo wakati huo, yeye. Naye ana dada mdogo, mdogo kwa miaka minne. Na kwa hiyo Becky ana macho ya samawati na kidogo ni mrefu, naye Sarah alikuwa na macho ya hudhurungi na kidogo ni mfupi. Kwa hiyo wote wawili walikuwa ni wasichana wa baba. Na mimi kweli ninawapenda watoto, naye Bwana alinipa watoto wazuri.

³ Na kwa hiyo walikuwa wakingojae kuniona. Nilipoingia, walitaka kucheza nami kidogo. Kwa hiyo mwasho wa usingizi ukaingia machoni mwao na ikawabidi kwenda kulala, yapata saa sita ama saa saba. Nayo ndege haikuwasili mpaka yapata labda saa nane ama tisa usiku. Basi nikaenda kulala, nisingeweza kulala. Nikatoka tu nikaingia sebuleni, nikaketi kitini. Ni mzaha kidogo, kwa namna fulani, ninaosema juu yao. Na ilikuwa ni. . .

⁴ Baada ya kitambo kidogo, kukapambazuka, naye Rebekah, hapa, akaamka, naye alijua kwamba nilipaswa kuwa nyumbani. Basi—basi akaangalia hapo na kumwona Sarah angali amelala. Kwa hiyo akaangalia na kuniona nimeketi chumbani, naye huyu hapa anakuja, kwa kasi tu alivyoweza, na kuruka pajani mwangu, mikono yote miwili. Na yapata wakati huo, Sarah, dada yake mdogo, akaamka. Vema, akaangalia, lakini Becky alikuwa tayari amemtangulia, kwangu.

⁵ Kwa hiyo kwa namna fulani ni kulinganisha hili na kanisa ambalo limekuwako kwa muda mrefu.

⁶ Basi Becky kidogo alikuwa ni mwembamba, mwenye miguu mirefu, naye angeweza kuketi pajani mwangu vizuri sana na miguu yote miwili imefika sakafuni. Alikuwa ameketi sawa, vizuri sana, mwajua.

⁷ Nasema hili kidogo kwa ajili ya ndugu yetu wa Kimethodisti hapa, amekuwa huku muda mrefu, mwajua, na akakua kidogo.

⁸ Vema, Sarah alikuwa kidogo ni mfupi. Nami sijui kama watoto wenu hufanya ama la; wangu hufanya. Mmoja ataninii, yule mkubwa atapata kitu kipya, kisha kitamwendea yule anayefuata, kisha kumwendea anayemfuata huyo. Basi—basi Sarah alikuwa amevaa pajama ya Becky. Nayo ilikuwa ni hizi pajama zenye miguu ya sungura walizozoea kuwa nazo, mwajua, kidogo ni kubwa, nayo miguu yake midogo isingeneea mle vizuri sana. Kwa hiyo akaanza mbio nyumbani.

⁹ Ndipo Rebekah akanikumbatia kwa mikono yake, kisha akageuka, akamwangalia Sarah, na akasema, “Sarah, dada yangu, ninataka ujue ya kwamba nilitangulia kufika hapa.” Akasema, “Nami nimempata baba wote na hakuna chochote kilichosalia kwako.” Vema, Sarah kidogo alijisikia kidogo amekwazwa, mwajua, kwa hiyo midomo yake midogo ikainama.

¹⁰ Basi kidogo inanikumbusha, labda makanisa ambayo yamekuwa safarini muda mrefu, mwajua. Wana ya ndani na nje yake yote, nao wanaweza kuketi chini na theolojia yote na kuielezea, na kuieleza katika Kiyunani, na kadhalika. Ninalinganisha hayo na Rebekah.

¹¹ Kwa hiyo basi Sarah anaangalia kila mahali, maskini midomo yake imeinama, ndipo akageuka na kuanza kurudi chumbani. Kwa namna fulani nilimkonyezea jicho na kumwashiria hivyo, na nikainua huo mguu wangu mwingine. Hilo ndilo tu alilokuwa akingojea. Huyu hapa anakuja, akaurukia mguu huu. Naye alikuwa...maskini miguu ilikuwa ni mifupi, mwajua, naye asingeweza kufikia sakafuni. Kidogo alikuwa shaghalabaghala. Kwa hiyo nilimzungushia tu mikono yangu, asije akaanguka, nikamkumbatia karibu nami. Akakilaza kichwa chake kifuani mwangu na kulala pale kidogo. Akamwangalia Rebekah. Akasema, “Basi Rebekah, dada yangu,” unaona, kasema, “Ninakutaka uelewe jambo fulani, pia. Huenda ikawa kweli kwamba ulitangulia hapo, na huenda unaye baba wote. Bali, ninakutaka ujue, baba amenichukua mimi wote.”

¹² Kwa hiyo, hivyo ndivyo karibu jinsi ilivyo. Mwajua, huenda nisijue yote ya ndani na nje. Bali mradi Yeye yu na mimi wote, hilo ndilo lote tunalojali. Acha Yeye atuchukue tu na kututumia jinsi anavyotaka kututumia.

¹³ Bila shaka ninathamini huku kukaa hapa, na ushirika huu mzuri miongoni mwa ndugu hawa wazuri, wahudumu, ushirikiano wote wa wafanya kazi wa kibinafsi, na kila kitu ambacho kimefanywa; kwa ajili ya Ramada, na kwa ushirikiano wao mzuri. Nami ninasikitika tu kwamba ni—ni siku nne tu. Mnaona, unafikia tu kuwajua watu, nao watu wanaanza kukujua, na halafu—halafu huna budi kuondoka, papo hapo wakati kweli jambo fulani lingeweza kufanywa ku—kumtukuza Mungu kwelikweli.

¹⁴ Na mambo yanayoendelea, huenda yamekuwa ni mapya kwa wengi wenu, na msingeweza kuyaelewa. Huwezi kulielezea jambo hilo katika usiku mmoja tu ama mbili. Na basi baada ya kutulia, bila shaka, ungeweza. Mambo mengi yeliendelea.

¹⁵ Ninyi wachungaji kumbukeni, ya kwamba, katika makanisa yenu, majuma kadhaa yajayo, kutakuwako na wanawake watakaowajia, wakisema, “Wajua, nilikuwa na shida ya wanawake. Imeondoka.” Mmoja, “Nilikuwa na shida ya tumbo. Imeisha.” Nisingeweza kuwaita wote. Ni kila mahali tu, imani ikiruka tu kila mahali.

¹⁶ Kwa mfano, dakika chache zilizopita, kulikuwako na mwa—mwanamume aliyekuja huku na—na kuweka mkono wake juu ya bega langu. Naye akasema... Nilimwangalia mtu huyo. Nikawaza, “Ninapaswa ku—ninapaswa kumjua mtu huyo.” Nilikuwa nimemwona mahali fulani.

Naye akasema, “Hivi unanikumbuka?”

Na, “Siamini ninakukumbuka.”

¹⁷ Kwa hiyo basi akasema, “Nilikuwa kwenye mkutano wako huko Saskatoon, huko Saskatchewan, katika miaka ya ’40, yapata mwaka wa ’42, ama kitu kama hicho. Nyuma kabisa, miaka mingi iliyopita.”

¹⁸ Nami nikasema, “Naam.” Nikawaza, “Nimemwona mtu huyo mahali fulani, bali siwezi kupakumbuka.” Na kwa hiyo tukaendelea, akaendelea, kuzungumza.

¹⁹ Katika dakika chache nikaanza kutambua, kwamba, siku chache zilizopita usiku, mkutanoni, kulikuwa na ma—mama, ninaamini kidogo alikuwa mwanamke mwenye mvi amesimama jukwaani.

²⁰ Na kama ningekuwa nimeangalia Mashariki, ambalo kwa kweli ni jambo la desturi kwamba ninapenda tu kuangalia Mashariki, maana Yeye yuaja kutoka Mashariki. Ninapobatiza, kwa kawaida mimi huwabatiza hivyo. Na inaonekana kana kwamba ninii... Daima kwenye upande wangu wa kulia, kwa sababu kila mara wakati Nuru hii inapoingia, Hiyo huja kutoka upande wa kulia. Na kwa hiyo daima mimi hujaribu kuwafanya watu waje kwangu kutoka upande wa kulia. Na ningekuwa nimesimama, kidogo namna *hii*, nadhani, kimahali sasa, jinsi hili jengo linavyokaa pale juu.

²¹ Ndipo chini upande wangu wa kushoto, niliona, akisimama karibu nami, mwanamke mwenye umri mdogo sana kuliko huyo mwanamke aliyekuwa amesimama mbele yangu. Naye alikuwa amevaa nguo za waridi. Ilikuwa ni tofauti na mwanamke aliyekuwa amesimama pale. Niliendelea kuona, kisha nikashuka. Nami...

²² Hakuna njia ya kulielezea. Inakubidi tu kuliamini. Hivyo tu.

²³ Nikaangalia chini. Kulikuwako na mama aliyekuwa ameketi chini *hapa*, moja kwa moja upande wangu wa kushoto, na kwa namna fulani alikuwa. . . Alikuwa na shida fulani. Kisha nikaangalia nyuma, na basi huyu hapa mwanamume amesimama karibu naye. Nikawaza, “Kuna jambo la kigeni.” Nami nilikuwa nikijaribu kuweka nia yangu kwa mwanamke huyo niliyekuwa nikimzungumzia.

²⁴ Kwa sababu, mnaona, labda, kama ukiangalia jambo likitukia, unaona, huenda linamwambia mwanamke *huyu* kile mwanamke *huyu* alikuwa nacho. Mnaona? Kwa hiyo, ninyi, ni ninii sana. . . Naye Shetani amekaa papo hapo kwa ajili ya kila nafasi awezayo. Ni neema ya Mungu tu, mnaona, kwamba Yeye huyaacha hayo yatendeke.

²⁵ Ndipo basi ni—nikaangalia. Nikamwona mwanamke huyu kwa namna fulani. . . Mmoja alikuwa ana umri mdogo sana kuliko huyo mwingine. Na mwanamke mmoja kidogo alikuwa. . . Alikuwa amevurugikiwa, hana akili timamu. Naye mwanamke huyo mwingine alikuwa na mateso ya namna fulani mabaya sana. Halafu basi mwanamume huyu. . .

²⁶ Ndipo nikaja kugundua, asubuhi ya leo, niliposimama hapa, huyo alikuwa ndiye mwanamume huyo. Basi nikasema, “Hivi wewe huna mke ambaye—ambaye ni mgonjwa, aliyerukwa na akili, anateseka, kitu kama hicho?”

Naye akasema, “Naam.”

²⁷ Nami nikasema, “Hivi yeye alikuwa mkutanoni, juzi usiku, naye akaketi mkono wangu wa kushoto, amevaa namna fulani ya nguo ya waridi ama kitu fulani?”

Kasema, “Naam.”

²⁸ Na huyo alikuwa ni yeye. Na hivyo ndivyo nilivyomtambua mtu huyo. Ninaamini ni. . . ninaamini niliandika jina lake. Ninakuwa, siwezi kukumbuka vizuri sana. Mchungaji M-a-c-k, aliketi papa hapa mahali fulani. Na hilo lilikuwa ni kweli, sivyo? Naye akaniambia, kasema, “Mke wangu, miaka mingi iliyopita, alikuwa katika mkutano wako, naye aliponywa mara moja kwa mwujiza uliokuwa ukimwelezea, na kumwambia juu ya shida zake. Naye aliponywa mara moja; na wengi, mara nyingi, ugonjwa adimu wa damu, na vidonda, na vitu kama hivyo.”

²⁹ Sasa, mnaona, kile kilichotukia, kama ningeweza kujaribu kuwaacha muone kile ninachomaanisha. Mama huyo alikuwa na imani. Mnaona? Nayo imani yake, alikuwa akiamini, hata hivyo labda pasipo na kadi ya maombi ama chochote kile. Bali alikuwa anaamini, na labda kwa nguvu kuliko huyo mama alivyokuwa, aliyekei mbele zangu.

³⁰ Na sasa, ninaamini, yeye alisema ya kwamba mke wake aliingia ndani. Na kama sijakosea, yule ndiye anayeketi pale pale

karibu na mwanamume yule. Na huyo ndiye mwanamke yule. Huyo ndiye yule mwanamke. Kumwangalia, huyo—huyo ndiye yule mama, vema.

³¹ Sasa, mnaona jinsi ne—neema ya Mungu, kwake? Mama huyo, kwa kweli, hakika aliamini kwa moyo wake wote. Nayo imani yake ilikuwa ni kubwa zaidi kuliko mtu huyo aliyekuwa amesimama hapa, ikamwendea huyo mama. Hakika, sasa, na kisha mtu huyo akaniuliza, akasema, “Ndugu Branham, hivi kuna chochote kibaya sana na mke wangu? Yeye atapona ama kitu fulani?”

Nikasema, “Bwana, sijui mimi.”

³² Mnaona, wewe ndiwe unayelisababisha ono hilo. Imani yako mwenyewe hufanya hivyo. Unaona? Imani yako hufanya hilo, si yangu. Ni wewe. Unaona?

³³ Yesu, akisimama pale mbele ya wale watu, naye mwanamke huyu akaligusa vazi Lake. Hata hakujua ni nani aliyemgusa. Akasema, “Ni nani aliyenigusa?” Sasa, Yesu asingesema lolote kwa kusema tu. Yeye, kweli, Yeye hakujua ni nani aliyemgusa. Basi akaangalia kote, kwenye kusanyiko mpaka akampata mwanamke huyo. Mnaona? Ndipo akamwambia kuhusu imani aliyokuwa nayo.

³⁴ Sasa, mimi, mimi nisingejua. Halafu basi wakati mwingine... Mnaona, hili halikuelezewa, nadhani. Lakini sasa, unaona, kile wewe, kile ulicho, shida yako, huyo ni Roho Mtakatifu akilifunua hilo. Na wakati mwingine ninaliangalia, linaingia giza, kivuli. Kamwe sisemi kitu, kwa sababu labda ni mauti. Na kwa hiyo ninasema tu, “Nenda zako, Bwana akubariki.”

³⁵ Na labda, kama wakikaa muda mrefu kutosha, wangojee tu pale, waone kile Bwana asemacho. Halafu basi hilo ndilo analosema Yeye. Sasa, hilo ndilo, ambalo ono limeonyesha shida yako, ama kile umefanya. Lakini basi kaa kimya na ungojee. Naona watu wakiondoka tu. Mnaona? Kaa kimya. Simama tu hapo na kungojea, na uone kile Yeye asemacho, na ndipo upate kujua.

³⁶ Kama likirudi, nami nione ono la vile utakavyokuwa. Hilo linaonyesha kile umekuwa. Halafu, kama ninaweza kuona kile utakachokuwa, utalion, daima ni BWANA ASEMA HIVI. Halafu basi, basi wewe liandike hilo, na uone kama hilo halifanyiki jinsi hiyo tu. Halitashindwa kamwe, ikiwa ni ono.

³⁷ Jambo ndilo hili. Nina imani. Kama ono likija, likaniambia, asubuhi ya leo, ya kwamba George Washington alikuwa anaenda kufufuka kutoka kwenye makaburi ya rais, kwamba niende kule nikamwite, ningeualika ulimwengu uje uone likutukia. Kweli. Halingeshindwa. Haliwezi kushindwa. Halijawahi kushindwa, na kamwe halitashindwa, mradi tu hujaribu kutumia dhana yako. Na sasa mara nyingi...

³⁸ Nafikiri sisi sote ni pentekote hapa, asubuhi ya leo. Sivyo? Mara nyingi, mahali nafikiri watu hupata shauku, mnaona, unapata dhana kwamba Bwana alisema *hivi-na-hivi*. Nawe unalisema, wakati kweli sivyo. Na hilo lingekuwa ni kosa kusema hivyo. Mnaona? Wewe subiri mpaka utakapojua ya kwamba Mungu hakika amenena, na itakuwa ni kamilifu kila wakati. Lakini kama umepata tu dhana ya kusema hivyo, huenda ukalisema, bali... Na unapofanya hivyo, hilo husababisha kitu kama uigaji wa kimwili. Na wewe, kweli, ndugu, dada, halimsaidii Mungu; linamzuia Mungu. Mnaona? Na labda Mungu anakuita kuwa sha—shahidi ama kitu kingine. Basi wewe dumu mwaminifu kwa kile Mungu anachokwambia ufanye. Kuwa shahidi wa kweli.

³⁹ Sasa, huu umekuwa ni mkutano mzuri sana, moja ya kundi zuri sana la imani nyuma yangu, la wahudumu, niliowahi kuketi pamoja nao. Nao watu huko nje katika wasikilizaji wamekuwa wazuri sana. Nami nasikitika tu kwamba inatubidi tu kufunga upesi sana namna hii. Bali natumaini, siku moja, yakiwa ni mapenzi ya Bwana, kurudi.

⁴⁰ Nadhani meneja hapa, Ndugu Borders, alitambulishwa kwa watu, nami ningetaka tu asimame. Ndugu Roy Borders amekuwa pamoja nami katika mapambano mengi makubwa. Naomba usimame, Ndugu Borders. Ni mnyenyekevu sana. Ndugu Borders hajui hili, bali limenirudia tena. Nitamwambia sasa. Na Ndugu Borders ni mtu mgonjwa. Inanibidi kukutana naye na kwenda—kwenda pamoja naye, baada ya ibada hii asubuhi ya leo. Ndugu Borders, natumaini halitakushtusha. Bali Bwana hana budi kumgusa Ndugu Borders, mara moja. Yeye ana kilango kinachofunga moyoni mwake. Hiyo ni kweli kabisa. Sijapata kuzungumza naye zaidi ya mnavyoniona jukwaani, bali hiyo ni kweli.

⁴¹ Nitamwambia mwanamke huyu wakati Roho Mtakatifu akiwa juu yangu, ndipo sina budi kuachia hapo, mnaona, maana anaanza tu kutenda kazi. Mama huyu anayeketi hapa sasa, akiangalia upande *huu*, yule mwanamume aliuliza. Si jambo zito. Ni badiliko la maisha, kukata hedhi tu, uchovu, kujisikia mchovu sana, na kuchanganyikiwa kabisa. Utakuwa sawa. Usiogope. Unaona? Hivyo ndivyo tu ilivyo. Sasa, Roho Mtakatifu mkuu, katika Uwepo Wake!

⁴² Nina msichana mdogo hapa ambaye mwanamume huyu ndiyo kwanza anene habari zake, nina mambo fulani yaliyoandikwa hapa chini. M—msichana mdogo alifanyiwa upasuaji, huko Phoenix, jana, figo likatolewa, ama kitu fulani, kutoka kwenye kanisa la Ndugu Outlaw, mtu ambaye yuko kila mahali niendako. Kama ni kwenye umbali wa maili mia moja, ama mia mbili, mtu huyu huhudhuria kila mkutano. Pia mmoja wa washiriki wa kusanyiko lake yupo hapa asubuhi ya leo. Pamoja na msichana mdogo aliyefanyiwa upasuaji, kwa ajili

ya kivimbe kwenye figo, na ni ya kufisha. Mungu pekee ndiye anayeweza kuokoa maisha ya mtoto huyo.

⁴³ Maskini msichana kiziwi ambaye Ndugu Jenkins amenena habari zake! Loo, kuna wengi mno walio wagonjwa na wahitaji.

⁴⁴ Na sasa, kabla tu hatujaenda kwenye sehemu ya kuzungumza ya ibada, ningetaka tu tuombe kwa dakika moja. Na tuinamishe vichwa vyetu. Na iwapo kuna haja zingine, inua tu mkono wako.

⁴⁵ Baba yetu wa Mbinguni, tunafundishwa, katika Maandiko makuu ya Kiungu, Maneno ya Mungu yaliyotiwa pumzi, yakaandikwa, ya kwamba, “Tutaketi pamoja katika mahali pa Mbinguni ndani ya Kristo Yesu.” Nasi tunajisikia kwamba asubuhi ya leo, kuona ku—kundi la watu wanaoelekea Mbinguni, waliofanyizwa kwa madhehebu yote mbalimbali, wemeketi pamoja. Kuwaangalia na kuona baadhi ya wanaume walio na umri mkubwa kuliko mimi, baadhi ya vijana wanaokuja; na kama tu vile majani na maua, na maumbile yote yanavyotenda kazi, ya kale huondoka na mabichi yanaingia. Baba wa Mbinguni, tunakushukuru Wewe kwa ajili ya Roho Mtakatifu, ambaye hutupa hakikisho hili kuu, ya kwamba Siku moja kuu tutakutana tena.

⁴⁶ Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya nguvu Zake kuu. Yeye husaidia udhaifu wetu. Na tunaomba kwa ajili ya msichana huyu mdogo ambaye—ambaye ametolewa uvimbe huu kwenye figo, na lina kansa. Bwana Mungu, mrehemu msichana huyu mdogo. Nafikiri, vipi kama alikuwa ni mtoto wangu? Ni kipenzi cha mtu fulani. Ninaomba kwamba utamponya. Naomba nguvu za Shetani ziondolewe kwake. Jalia mtoto huyo aishi kwa utukufu wa Mungu.

⁴⁷ Bariiki, naomba, asubuhi ya leo, yule msichana mdogo kiziwi, aliyetajwa. Naomba kwamba Wewe utarudisha kusikia kwa huyo msichana mdogo, msichana mdogo wa Jenkins.

⁴⁸ Naomba, Baba wa Mbinguni, kwa ajili ya Ndugu Borders, ndugu yangu wa thamani, tunapooni Shetani akijaribu kumwondoa hudumani. Mungu, tunamdai kwa ajili ya Ufalme.

⁴⁹ Pia tunaombea haja hizi zote maalum. Na kwa ajili ya mama huyu ambaye hivi majuzi usiku akisimama kule, ile imani ikipanda, sasa Wewe umemwelezea, Bwana, na sasa itakuwa sawa. Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya jambo hili. Tunaomba ya kwamba Wewe utaendelea kuwa pamoja nasi.

⁵⁰ Bariiki wahudumu hawa. Bariiki wote ambao wamesaidia; wanamuziki, maskini waimbaji hawa wanne walioimba, na waimbaji wanne kutoka kwenye kanisa lile kule, hao vijana wazuri, kwani yule mama alituambia nyimbo maalum. Na mambo haya yote, Bwana, ni—ni mengi sana kukumbukwa niani mwetu, bali Wewe unayajua yote.

51 Kwa ajili ya Hoteli hii ya Ramada, kwa ajili ya yule mtu mzuri aliyesimama hapa dakika chache zilizopita, na kusema, “Mungu awabariki.” Mungu, tunaomba kwamba itamrudia, na kwamba yeye, Bwana, atajazwa na Roho Mtakatifu, awe shahidi mkubwa ulimwenguni, wa Yesu Kristo, jambo kuu kuliko yote ambalo lingeweza kutukia, Baba.

52 Sasa tunaomba ya kwamba Wewe utambariki Ndugu Tony na watu hawa wazuri hapa, hata wakiwa ni washiriki walei wa kanisa. Na, hata hivyo, wanajaribu, hawa Wafanya Biashara, kujiunga pamoja wenyewe, kufanya ushuhuda mwingine. Mungu jalia jitihada zao, wajazwe na Roho na kutambua wapate kujua la kufanya na jinsi ya kufanya kutenda kwa ajili ya Bwana Yesu.

53 Bariiki Ujumbe asubuhi ya leo, Bwana, ninaponena. Pia naomba ya kwamba Wewe utautia mafuta kwa baraka Zako. Na wakati tutakapoondoka, tunaweza kusema kama wale waliotoka Emau, “Mioyo yetu iliwaka njiani.”

54 Halafu, Baba, kukiwako na mtu asiyeokoka hapa ndani, mmoja asiyejua Wewe, ama mfuasi tu wa kanisa, jalia nguvu kuu za Roho Mtakatifu ziwafunulie haja yao leo hii ya wokovu kupitia njia ya Mungu iliyoandaliwa, njia pekee, Yesu Kristo, kwa kuwa tunaomba hayo katika Jina Lake. Amina.

55 Ninawashukuru tena. Jambo moja nililosahau kutaja, muda mfupi uliopita. Wao...Ndugu Tony, wakati akitoka kwenda kwenye motokaa jana usiku, alisema...Nilisema, “Kamwe siangalii...” Nimekuwa hudumani sasa miaka ipatayo thelathini na mitatu. Nilifanya uchungaji kwenye maskani huko Jeffersonville kwa muda wa miaka kumi na saba, kamwe sikuwa na mshahara hata peni moja. Na kamwe sikuchukua sadaka, siku zote za maisha yangu. Kamwe sikuchukua, kamwe sikusudii kuchukua moja. Na jana usiku Ndugu Tony alisema walikuwa...Nikasema, “Mlikidhi matumizi?”

56 Maelewano, wakati nilipokutana na ndugu huyu mwema, Brock. Na hivi nilitamka hilo vizuri, “Brock”? Na Ndugu Gilmore, na baadhi ya ndugu wengine kule juu, hivi majuzi usiku. Nilisema, “Sasa, waliuliza juu ya hali ya fedha.” Nikasema, “Chochote tu yalicho matumizi, hakuna lingine.”

“Vema,” akasema, “tunataka kukuchukulia sadaka.”

57 Nikasema, “La, la. Msifanye hivyo. Na—napata—napata dola mia moja kwa juma kutoka kanisani mwangu na hilo linashughulikia jambo hilo,” nikasema, “Mimi, yote ninayohitaji. Mimi, sihitaji kitu, mnaona.” Mimi, ninawazia juu ya kule upande ule mwingine, Kule, kitu fulani Kule. Nami ninajua ya kwamba—ya kwamba nilijaribu kuweka huduma yangu...

58 Wengi sana wamekuja, na meneja, wakisema, “Ndugu Branham, inapaswa kuwa kwenye nuru angavu.”

59 Naye rais wa Four Rose Whiskey alikuwa kule kwetu, hapa wakati fulani uliopita, naye alimleta binti yake. Naye akasema, loo, msichana huyo mdogo alitaka kuponywa. Naye alisema alikuwa amesikia habari zake, na alikuwa akienda kufanyiwa upasuaji. Na kwa hiyo wakasema... Loo, alitaka kuja huku. Hakutaka kufanyiwa upasuaji.

60 Vema, alingia moja kwa moja upesi wakati nikihubiri, akitaka kuombewa wakati uo huo, ilibidi iwe ni wakati uo huo. Vema, sasa, asingeweza kungojea. Mama yake alikuwa akimtafuta. Kwa hiyo mama akaingilia nyuma ya kile chumba, akaketi akiwa na huo mtazamo wa kiburi. Kwa hiyo basi tukaja, tukamwomba msichana huyo mdogo na kurudi.

61 Vema, siku kadhaa baadaye, daktari alikuwa amesema, kasema, "Vema. Ni ujinga mtupu." Kasema...

62 Lakini yeye akasema, "La, najisikia vizuri. Sina ugonjwa wa kidole tumbo. Ni mzima na mwenye afya."

63 Kwa hiyo basi wakaendelea, siku nne ama tano. Baada ya kitambo... Mnaona, kama tu nilivyoliezea, baada ya yapata saa sabini na mbili, dalili hiyo hujirudia tena kama kweli uliponywa, unaona, uponyaji. Sizungumzi juu ya miujiza. Nao ukajirudia kwa sababu kidole tumbo kilianza kuvimba. Ndipo daktari akasema, "Sasa, mnaona? Sasa afadhali uende ukamlete huyo mhubiri mtakatifu anayejibingirisha tena."

64 Kwa hiyo basi, asingeweza kufanya upasuaji. Lakini, bila shaka, wakati kukiwako na dola elfu moja mia tano zinazohusika, a—a—angeweza kuufanya. Alisema asingeufanya, bali aliufanya. Ilitokea rafiki yangu alikuwa kwenye wataalamu hao, ambapo, wakati walipokiondoa, walipompasua msichana huyo, kukiondoa hicho kidole tumbo, hapakuwapo na shida yoyote. Mnaona? Walimpasua bure. Walikiacha tu kidole tumbo hicho mle, maana hata hakikuwa kimeathirika kwa njia yoyote. Basi huyo daktari akaja, akaniambia juu yake, rafiki yangu kwenye wataalamu hao, aliyesaidia kufanya upasuaji.

65 Sasa mnaona kilichokuwa. Mtoto huyo alikuwa amesisimkwa sana hata hakujua jinsi ya kuishikilia imani hiyo. Mnaona? Na hapo hatupati nafasi ya kuelezea jambo hilo. Basi hilo lilifanya nanii... Daktari rafiki yangu alimwambia yule mama, na kusema, "Kidole tumbo kingali mle." Wakasema, "Alikihitaji hicho kidole tumbo, na hakikuwa kimeathirika. Hapakuwapo na kitu kukihusu, hata kidogo, ni cha kawaida tu kabisa, waridi; ninii tu, loo, jinsi kinavyopaswa kuwa."

66 Basi mama yake akawa mwaminio. Ndipo akaniambia, "Kile kinachopaswa kufanywa, ni, huduma yako, sio kuketi pembeni pamoja na kundi la—la watu tu wa kawaida. Inapaswa kurushwa kote nchini kila mahali, inapaswa kuwa kwenye vibao vya matangazo." Sasa hivyo ndivyo tu ibilisi anavyotaka. Hiyo ni kweli. Mnaona? Lakini, la, siitaki namna hiyo.

⁶⁷ Ni—ninaitaka ili kwamba ninaweza tu kutembea mahali popote, kufanya lolote. Popote Bwana aitapo, hapo ndipo ninapotaka kwenda. Mahali tu ambapo Yeye anaiweka tu nyenyekevu, na tuache Bwana atupeleke popote anapotaka kutupeleka.

⁶⁸ Na sasa, kwenu ninyi watu, kama nyinyi... ambao mmeombewa, kama nyinyi... Baada ya yapata saa sabini na mbili, kuoza kunaanza. Tunajua hilo. Kuoza huanza baada ya saa sabini na mbili. Kama kitu fulani kikijirudia... Kama kweli unaamini hilo, kwa moyo wako wote, hakuna kitu kitakacholikomesha. Wewe liamini, kwa vyovyote vile. Dumu nalo moja kwa moja. Itakuwa sawa. Usininii...

⁶⁹ Lakini huwezi kulipumbaza sasa. Inakupasa kulijua kweli, kwamba limetendeka. Unaona? Kuna tofauti kubwa sana kati ya tumaini na imani. Tumaini linalitumainia tu hilo. Imani inajua limetendeka. Kwa hiyo, hiyo ndiyo tofauti.

⁷⁰ Sasa, asubuhi ya leo, sitaki kuwaweka. Ni saa nne tayari, na, mnaona, imepita kama dakika sita, kwa saa hii ya mkono ambayo Billy alinipa.

⁷¹ Na sasa ninataka kusoma kifungu kutoka kwenye kitabu cha Isaya, mlango wa kwanza, kwa ajili ya maelezo machache tu. Nami ninayo Maandiko yaliyoandikwa hapa, ambayo huenda nikayarejea. Na kuwaweka tu yapata dakika thelathini, ndipo tutakuwa tayari kuondoka, Bwana akipenda. Isaya, mlango wa kwanza na kifungu cha 18.

Haya, njoni, tusemezane, asema BWANA, dhambi zenu zikapokuwa nyekundu sana, zitakuwa... nyeupe kama theluji, zikapokuwa... nyekundu kama bendera, zitakuwa nyeupe kama sufu.

⁷² Sasa, Bwana na aongeze baraka Zake kwenye kusomwa kwa Neno Lake. Nami ninataka kuzungumza juu ya somo la: *Makongamano*. Kufanya kongamano!

⁷³ Bwana, libariki Neno sasa, na jalia mbegu zianguke mioyoni mwetu, ambamo tuna haja. Pia, Bwana, jalia wangu ufunguke, pamoja na kila mmoja hapa, ili tupate kuifahamu saa tunayoishi na yale tunaopaswa kufanya. Katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

⁷⁴ Tukizungumza juu ya makongamano, tu—tunasikia mengi sana juu yake siku hizi. Kila kitu ni kongamano. Na, kusema kweli, hilo ndilo tulilo ndani yake hapa asubuhi ya leo, ni kongamano. Nasi tunasikia mengi sana juu ya hayo, na mahali pengi sana mbalimbali ambamo yanafanyiwa, mambo mengi sana yanayotimizwa kwa makongamano. Nafikiri ni jambo tunalopaswa kufanya, ni kufanya kongamano. Na kwa kawaida, wakati yanapofanywa, katika wakati wa dharura. Kwa kawaida wakati kukiwa na dha—dharura, ndipo mnafanya kongamano.

Unaitisha kongamano la haraka. Nasi tunaliwazia kwa misingi hiyo.

⁷⁵ Sasa, hapa, wengi wenu mnaweza kukumbuka ninii... kwa mfano, lile kongamano tulilokuwa nalo katika hali ya hatari ya ulimwengu, wakati Ujerumani na ulimwengu wote walipokuwa vitani, wakati Rais Roosevelt alipokuwa rais wa Marekani. Na—na kulikuwako na wale wengine wanne wakuu, wanavyoliita. Walifanya, kile walichokiita “Kongamano la Mabingwa Wanne,” la Churchill. Nao wakakutana pamoja, na ikawabidi kufanya kile walichokiita Kongamano la Mabingwa Wanne wa ulimwengu huru, kwa sababu kwamba iliwabidi kuja pamoja na kuleta mawazo yao pamoja, na kufanya mkakati wa mahali fulani, kwa sababu adui alikuwa anakaribia, na hana—hana budi kukomeshwa.

⁷⁶ Halafu wa—walikuwa wakutane, kusudi waweze, lile kundi lililo na hekima kuliko yote. Ndipo mmoja angepata wazo la mmoja, na wazo la mwingine, kisha wayaunganishe pamoja, ndipo waone wanachopata. Hilo lilikuwa ni lile Kongamano la Mabingwa Wanne. Na mahali wanapopaswa kushambulia, mahali wanapopaswa kuyaweka majeshi yao, lile fulani, kama vile lile Jeshi la Tano, na Jeshi la Nne, na Jeshi la Kumi, na kadhalika, na jinsi wangeweza kufanya kazi pamoja, na mahali ambapo adui alikuwa na ngome zake.

⁷⁷ Na kama mkitambua, daima wao hujaribu kuushambulia huo uti wa mgongo. Huo ndio tegemeo. Na daima ni, kumshambulia adui! Kama unataka kumwua, huna budi kumpiga sehemu iliyo muhimu sana. Usipofanya hivyo, hutamwua. Na kwa hiyo basi, jambo moja tu la kufanywa.

⁷⁸ Ni kama tu kuandaa mkutano. Kama tungeweza kuuchukua U—Ufalme wa Mungu, kama vile watu wamesema mara nyingi, katika huduma, na kama kumnukulia tena yule mwanamke, kasema, “Kama ungaliweza kuwachukua na kuwakusanya mabingwa pamoja, wenye akili nyingi, na kuliweka pamoja, kisha mshambulie kutoka papo hapo.” Lakini, unaona, unashambulia kitu kisichofaa. Unaona?

⁷⁹ Kama ninaweza kuwaleta wahudumu pamoja, kama ninaweza kuwaleta pamoja watu waliookolewa na Mungu, na kuwafanya waone nguvu zilizoko katika Kristo Yesu, kwamba—kwamba Yeye kweli anaishi mioyoni mwetu, na anaweza kujua mawazo ya nia, na kutabiri, na kubashiri, na—na kulifanya kamilifu, basi hao wahudumu watavuviwa nao watalipeleka kwa watu wao. Basi mnaona ninachomaanisha? Hapo ndipo mahali pa kushambulia, ambapo bunduki zimewekwa sasa.

⁸⁰ Basi katika Mabingwa hao Wanne walifanya kongamano hilo mashuhuri. Kisha tulikuwa na kongamano lingine lililoitwa Kongamano la Geneva. Nina hakika wengi wenu mnakumbuka wakati ilipowabidi kufanya li—lile Kongamano la Geneva. Kisha

kulikuwako na jingine lililoitwa Kongamano la Paris, wakati walipokutana Paris. Ni daima tu, wakati wote, kongamano baada ya kongamano baada ya kongamano, kukutanika pamoja, kwa sababu haja ni kubwa katika maisha ya kitaifa. U—ubongo wa ulimwengu unaonekana kuchaganyikiwa sana hata hujui ni wapi, nini la kufanya. Na ulimwengu mzima unaogopa mno sasa hivi.

⁸¹ Inanikumbusha kuhusu mvulana mdogo akienda nyumbani katika usiku wenye giza, akipitia makaburini, akipiga mbinja. Anapiga tu mbinja kwa nguvu awezavyo, kwa sababu anajipumbaza tu, mwenyewe. Ha—ha—hataki kuwazia kwamba anaogopa, bali anapiga mbinja kujaribu kujituliza. Lakini chini kabisa, anaogopa, “Nyuma ya kila jiwe la kaburi mna jini.” Ama, unaona, yeye ana woga, naye anapiga mbinja apate tu kujituliza kwa namna fulani.

⁸² Na hiyo ndiyo sababu tunao uozo mwingi sana leo hii kwenye redio na televisheni, wa watu, kama watu walio na vipaji, waimbaji kama vile Ernie Ford na Elvis Presley, hao wavulana ambao wanauza haki zao za mzaliwa wa kwanza kwa mlo wa dengi. Wanaenda huko nje, na yote unayopaswa kuwa ni mcheshi, ama kufanya mzaha fulani, ama—ama kitu kama hicho, kuuchekesha umma wa Marekani. Wakati, unajua unajaribu tu kuwatuliza; na unajua, nyuma ya hayo yote, tunajua ya kwamba hukumu imekaribia. Hiyo ni kweli. Afadhali tukabiliane nayo. Tuko kwenye mwisho wa safari, ndugu zangu. Na mizaha yote ya Ernie Ford, na roki za Elvis Presley, na upuuzi huu wote, ni karamu nyingine ya Nebkadreza. Haitafaa kitu hata kidogo. Hukumu itapiga.

⁸³ Taifa hili limefikia mahali pale pale kama Sodoma na Gomora. Naye Mungu mwenye haki, akiiacha nchi hii iendelee na yale inayofanya sasa, kama Mungu mwenye haki Yeye angewajibika kimaadili kuifufua Sodoma na Gomora na kuomba msamaha kwa kuwateketeza, hiyo ni kweli, kama tutapita bila hukumu. Bali, kumbukeni tu, inatujia sisi.

⁸⁴ Kimbilieni kwenye ule Mwamba upesi mwezavyo. Msiliahirishe. Msiangalie kile hawa wote, kujiunga tu na kanisa na kanuni ya imani na kadhalika. Fanya kama hawa ndugu wa Kimethodisti hapa: kimbilieni kwenye ule Mwamba mpaka kitu fulani kirudishe mwangwi, hata umwone Kristo akiakisi. Huenda ikalazimu kukupiga kidogo. Katika nyakati za kale za Biblia, wakati wao, nanii . . .

⁸⁵ Siku hizi, hapa katika jimbo hili la dhahabu la Arizona, zamani za kale, wana wayeyushaji sasa wa kuyeyusha chuma na kimbwi, kinachoitwa dhahabu ya mjinga, na kuiyeyusha hiyo kutoka kwenye dhahabu halisi, kwa kiyeyushi.

⁸⁶ Zamani za kale, njia pekee waliyokuwa nayo ya kuitenganisha ilikuwa ni mtwangaji, kuigonga dhahabu kwa

nyundo, kama Wahindi wanavyoitwanga. Na njia pekee ambayo mtwangaji alijua ya kwamba dhahabu hiyo ilikuwa tayari, ilikuwa ni wakati alipotwanga uchafu wote kutoka kwake. Naye angeitwanga, na kuigeuza, na kuipiga, na kuipiga, mpaka uchafu wote ukatoka. Wakati alipojiona mwenyewe amekisiwa kwenye dha—dhahabu, alijua basi kwamba uchafu wote, na chuma, na vitu vya kigeni vilikuwa vimetoka kwenye dhahabu hiyo.

⁸⁷ Na hivyo ndivyo Mungu anavyojaribu kulifanya kanisa Lake, ni kulitwanga mpaka kanuni zote za imani, na upuuzi, na ulimwengu wote, umetwangwa ukaondoka kwake, mpaka linayaakisi Maisha ya Yesu Kristo. Kumbukeni, enyi kanisa! Ndiyo kwanza nitoke kwenye mkutano mkubwa nyumbani, ambako ile Mihuri sita, na ule Muhuri wa sita... ama, Mihuri saba. Nao huo wa sita ulikuwa ni utakaso wa kanisa. Kanisa, bila shaka, linapitia kwenye kile kipindi cha Dhiki kuu kwa ajili ya kutakaswa kwake. Bali, Bibi-arusi ananyakuliwa, ndiyo tofauti kati ya Bibi-arusi na kanisa.

⁸⁸ Natumaini siingilii mafundisho hapa sasa. Kama nikisema chochote ambacho huamini, mbona, fanya tu kama nifanyavyo wakati nikila sambusa ya cheri. Na—napenda sambusa ya cheri. Lakini ninapofikia mbegu, kamwe siitupi hiyo sambusa; naitupa tu hiyo mbegu. Kwa hiyo wewe fanya vivyo hivyo. Unapokula kuku, unapofikia mfupa, humtupi kuku, unautupa tu mfupa. Kama nikisema jambo usiloamini, tupilia tu mbali mfupa huo, unaona.

⁸⁹ Sasa, bali kuna hali za dharura, na migogoro inaendelea, na daima inamwita rais kwenye ile ya mwisho, kwenye makongamano, nao hawana budi kukutanika kwa ajili ya *hili* ama *lile*. Nayo Kuba italipuka, ndipo inawabidi kuitisha kongamano. Na kitu fulani kingine kitalipuka, inawabidi kuitisha kongamano. Karibu, yote tunayosikia, ni kongamano.

Wanafanya nini kwenye kongamano? Linapangwaje?

⁹⁰ Jambo la kwanza, wanaitana pamoja, kisha wanachagua mahali fulani. Huko Geneva, nimekuwa huko. Hapo ni ma—mahali mashuhuri, panapopendeza. Na kwa kawaida wao hujaribu kuenda kwenye mahali panapovutia, kusudi waweze kwenda kule, na kisha wanapachagua mahali hapa, wanaita watu wote mashuhuri mahali hapa pamoja. Na kufanya ninii... Sijaliandika hapa chini. Mahali hapo palikuwa wapi huko Uswisi, tulienda chini kule, Billy? Ambapo wao... Hiyo ilikuwa ni huko Geneva, sivyo? Nami nafikiri ilikuwa ni nchi ya kupendeza. Sikuandika ji—jina la kongamano hilo, bali ninakumbuka kuwa kule. Nao wanakutana na kupata mahali hapa, nao wanachagua pazuri wawezapo, na kupashughulikia.

⁹¹ Sasa, hayo ni ya ulimwengu. Na kila kitu kilicho kibaya, kila kitu kilichoko ulimwenguni, ni kibaya, ni mfano wa kilicho

sahihi.

⁹² Sasa, dhambi yenyewe ni haki tu iliyopotoshwa. Sasa, kuna Muumba mmoja tu, na huyo ni Mungu. Naye Shetani si mwumba. Yeye ni mpotoshi tu wa uumbaji asilia. Uongo ni Kweli iliyowakilishwa vibaya. Uzinzi ni tendo sahihi likitumiwa vibaya. Kila kitu daima ni upotovu wa kilicho sahihi. Shetani anaweza kupotosha bali hawezi kuumba. Mnaona? Na—na sisi tunakumbuka hilo, ya kwamba ubaya, uongo, ama kitu chochote kilicho dhambi, ni haki iliyopotoshwa. Na kwa hiyo tunaona ya kwamba Shetani daima huchukua mfano, kwa ajili ya kile anachoenda kufanya, kutokana na kile Mungu amefanya.

⁹³ Kwa mfano, kama vile watu wengi wakiona mkutano, wanasema, “Ni kuwasiliana kimawazo. Ama, ni ninii. . . Huyo mtu ni, aliitwa nani? Simoni, yule mchawi, na—na kitu kama hicho.” Mnaona? Kwa nini? Unapomwona mshirikina ama pepo akitenda kazi, ni upotovu tu wa kitu halisi cha kweli alichopo nacho Mungu. Hiyo ni kweli. Mnaona?

⁹⁴ Nao wanadamu wanapaswa kuwa, wanapaswa kujua vya kutosha, na wa kiroho kutosha, ili waweze kupambanua kati ya kilicho kweli na uongo. Uliwahi kusikia kuhusu mshirikina akitoa pepo, na—na kuwaponya wagonjwa, na kuhubiri Injili? “Na kwa matunda yao wanajulikana.” Mnaona? Wana kituo kidogo pale pembeni mahali fulani, na kusoma kiganja cha mkono wako, na kubahatisha mambo manne ama matano, na dazani moja yake ni uongo. Haya basi, unaona. Huo ni upotovu tu, kujaribu kuzivutia nia za watu, zisizotulia, ziondoke kwenye Roho Mtakarifu wa kweli, aliye halisi, ambapo tunaweza kuketi pamoja katika mahali pa Mbinguni, na Kristo atufunulie kile tunachopaswa kufanya.

⁹⁵ Makanisa yanapaswa kuwa hivyo. Watu wanaonena kwa lugha. . . Ni—ninataka tu kusema hivi, kwa kuwa mimi ni baba yenu, tuseme. Nitajifanya hivyo asubuhi ya leo. Mnaona? Tunalo jambo kuu. Bali ni—ni. . . ninaamini kwamba halijawakilishwa tu vizuri. Mnaona? Nalo litajiuza lenyewe ikiwa litawakilishwa vizuri. Sasa, nafikiri kuna wengi wa hawa Wamethodisti, hawa Wabaptisti, na Wapresbiteri, wangetaka kuwa na Hili. Bali ni jinsi tunavyoliwasilisha Hilo kwao. Mnaona?

⁹⁶ Sasa, kama ukimwona jamaa fulani huko nje akijenga nyumba, naye ana nyundo na anapigilia misumari ndani ya nyumba. Uende. Nawe una mtambo unaoweza kupigilia nusu kipipa cha misumari mle, “Rruut.” Unapigilia tu misumari namna hiyo, upesi maradufu, na kazi bora zaidi. Kama ukimwendea, umwambie, “Aa, unafanya nini? Wewe ni wa mtindo wa kale. Hutaki kufanya hivyo. Hiyo ni njia mbaya. Hapa, ninao mtambo utakaofanya jambo hili.” Upesi sana, umeharibu biashara yako. Ninyi wafanyabiashara mnajua hilo. Umeiangamiza biashara yako. Jambo la kufanya ni kwenda

na kumjivunia, jinsi—jinsi anavyoweza kujenga vizuri, halafu umwonyeshe tu bidhaa hiyo. Kama ni nzuri hata kidogo, itajiuza yenyewe. Ninyi wauzaji mnajua hilo.

⁹⁷ Nanyi mnajua hakuna kitu kilicho bora zaidi ya ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hakuna kitu bora zaidi alichopewa mwanadamu, kutoka Mbinguni, nje ya Roho Mtakatifu. Lakini, mnaona, sisi—sisi tunajaribu kumwangusha jamaa huyo mwingine. Hebu tujaribu kumwinua kidogo, na kumkumbatia, na kumfanya ifahamike kwamba blanketi hii inaenea kote kitandani. Mnaona? Na ufanye kongamano la namna hiyo, unaona. Mpe nafasi kidogo, pia, lakini hata hivyo ame—amejitahidi.

⁹⁸ Sasa, lakini, mnaona, mara nyingi makanisani mwetu, tunawaruhusu watu kusimama tu hata wakati unapohubiri, na kunena kwa lugha, na unapofanya wito wa madhabahuni, mtu fulani ananena kwa lugha, na mtu fulani kuninii, na kutoa tafsiri. Angalau, mmoja wao, ninaamini, ninaamini mtu huyo kweli ananena kwa lugha. Bali ninaamini huyo mwingine, kwa namna fulani, anatabiri, maana, wengine watanena kwa lugha, labda kwa dakika tano, na huyo mwingine atoe maneno manne ya ufasiri. Mnaona? Haina budi kuwa ni kwa sauti ile ile, mwinuko ule ule na mshuko wa sauti.

⁹⁹ Halafu basi, tena, kama wakilisema, na lisitimie, basi mwondoeni huyo roho mchafu kwenu. Hamtaki hilo. Katika maskani yangu, wakati mtu anaponena hivyo, ni afadhali awe nalo. Linaandikwa chini. Lisipotimia, wanamwondoa huyo roho mwovu kutoka kwao. Halina budi kuwa kamilifu, sio marudio. Yesu alisema, “Msipayuke—payuke kama wafanyavyo makafiri.” Halina budi kuwa ni jambo la moja kwa moja kwa mtu fulani, ama kulisaidia kanisa, ama kuisaidia huduma. Hilo linaandikwa chini moja kwa moja. Na kama sivyo... Nao hao watu wanaonena kwa lugha, na hizo karama kuu kuusaidia mwili wa Kristo, wanakutana saa kadhaa kabla hatujapata kufika kule, naye Roho Mtakatifu anatenda kazi kupitia wao. Ndipo yanawekwa kwenye dawati, nasi tunatangaza vile wamesema hapa. Basi kama hayatimii kabisa kama ilivyosemwa yatatimia, basi hawawezi kufanya hivyo tena mpaka roho huyo mwovu amewatoka.

Mnasema, “Vema, Ndugu Branham, hivyo?”

¹⁰⁰ Vema, angalieni. Nami inanibidi kusimama hapa. Nisengeogopa, kwa sababu ni Mungu. Halina budi kuwa ni kweli, kila wakati, hapa. Na linapaswa kuwa ni kweli, huko nje, kila wakati. Ndipo wakati watu wanapoyaona mambo hayo yakitimia, basi wataamini.

¹⁰¹ Kile kanisa la Kipentekoste linachohitaji, asubuhi ya leo, ni kongamano zuri. Hiyo ni kweli kabisa. Madhehebu yote, la—la umoja, uwili, utatu, unne, na wengine wetu wote, na church of

God, Assemblies of God, sisi sote tuje pamoja na kushauriana mambo haya, hiyo ni kweli, na kulifanya kanisa kuendelea.

¹⁰² Mradi tu Shetani anaweza kuwafanya mwendeleo kushambuliana nyinyi kwa ninyi, yeye anaketi tu kitako na kusema, “Ndugu, hata hainibidi kupiga vita.”

¹⁰³ Lakini kama tungeweza tu kuja pamoja, na kumtazamia Mungu, kama ndugu, kisha tupige hatua, tuna silaha, tumeungana. Haikubidi kubadilika, na mmoja aende kwa kanisa moja. Na kufanya ji—jinsi utakavyo. Tofauti hizo ndogondogo mnazofanya si tofauti hata hivyo. Mungu alimpa kila mmoja wenu Roho Mtakatifu. Kwa hiyo Biblia ilisema, “Mungu huwapa Roho Mtakatifu wale wanaomtii Yeye.” Kwa hiyo hakika mtu fulani amemtii Mungu.

¹⁰⁴ Lakini jambo ni, mradi tu Shetani anaweza kudumisha tofauti hizo ndogondogo, hilo ndilo linaloliweka kanisa katika vurugu kama liliyomo leo hii. Hebu na tusahau jambo hilo na tuje pamoja.

¹⁰⁵ Kumbukeni, ndugu huyo mwingine yuko tu ndani ya Kristo kadiri tulivyo sisi. Hakuna watu wakubwa, hakuna watu wadogo, hakuna wakubwa. Sisi ni watoto. Tu mmoja katika Kristo. Na tufauti zetu ndogondogo hazileti tofauti yoyote. Kama Becky anataka nguo ya samawati, naye Sarah anataka nyekundu, wote wawili wanapata nguo. Hilo—hilo... Mnaona ninalomaanisha? Kwa hiyo haiwapasi kubishania hilo. Kwa hiyo nafikiri hilo ndilo tu—tunalopaswa kufanya kwa kweli.

¹⁰⁶ Sasa, tukinena kuhusu makongamano ya ulimwengu, kwenye migogoro ya ulimwengu. Mwajua, Mungu amekuwa na makongamano, pia. Tunawazia juu ya lile la Paris, na Geneva, na lile la Mabingwa Wanne, na makongamano mengine mengi. Hebu tuwazie baadhi ya makongamano sasa ambayo Mungu alikuwa nayo, ambayo haya yalikuwa ni mifano kutokana na, na yale Mungu amekuwa nayo.

¹⁰⁷ Na—nafikiri ya kwamba kongamano la kwanza, ninaloweza kuwazia sasa, tukinena Kimaandiko, nitaliita kongamano la Mungu la Edeni. “Mungu alimfanya mtu kwa mfano Wake Mwenyewe, katika mfano wa Mungu Yeye alimwumba; mwanamume na mwanamke Yeye aliwumba.” Walikuwa ni watoto Wake wapendwa. Nao waliwekwa kwenye msingi wa uhuru wa kujichagulia.

¹⁰⁸ Maskini kafiri wa kale amesema, mara nyingi, “Kwa nini Mungu mwenye haki afanye kitu kama hicho, na kusababisha mateso yote yaliyoendelea kote katika wakati?”

¹⁰⁹ Mungu hakufanya jambo hilo. Mwanadamu alilifanya, mwenyewe. Mungu hakupenda yeye afanye hivyo.

110 “Vema basi, kama Mungu alikuwa mwenye nguvu zote, kwa nini Yeye akaliacha hata litukie? Kwa nini Yeye hakumfanya mtu mkamilifu?”

111 Kwa sababu, hapo mwanzo hapakuwapo na kitu ila Mungu. Na ndani ya Mungu kulikuwa na sifa, sifa Yake kuwa Mwokozi. Tunajua ndivyo ilivyo. Yeye ni Mwokozi, na hiyo ilikuwa ndani Yake. Na hapakuwapo na chochote kilichopotea, kipate kuokolewa. Ndani Yake mlikuwamo na sifa za kuwa Baba, na hakukuwako na chochote angaliweza kuwa baba yake. Ndani Yake mlikuwamo na sifa za kuwa mponyaji. Hapakuwapo na kitu kilichopotea, hakuna chochote kigonjwa. Kwa hiyo jambo pekee ambalo Yeye angaliweza kufanya lilikuwa ni kumfanya mtu juu ya msingi wa uhuru wa kujichagulia, akijua kwamba angefanya jambo hilo. Mungu hakufanya hivyo, Mwenyewe. Mwanadamu alilifanya, mwenyewe.

112 Na wewe uko vivyo hivyo asubuhi ya leo. Unaweza kuukubali Uzima ama kuukataa Uzima. Lakini Mungu alimfanya mwanadamu hivyo, kwamba angeweza... akijua angefanya hivyo, pasipo kutaka yeye afanye hivyo, bali akijua angelifanya, kusudi liweze kuonyesha sifa Zake. Kwa hiyo hakuna chochote kilichopitwa na wakati. Kila kitu kinadunda hasa kabisa kulingana na saa kubwa ya Mungu. Mnaona? Na hili huonyesha tu sifa Zake, kuwachagua watoto Wake ambao kweli wanampenda na wanamwamini. Na kila mtu ana haki sawa.

113 Mungu akiwa asiye na kikomo, alijua tangu mwanzo kitakachokuwako na ambacho hakitakuwako. Kwa hiyo basi Yeye hakutaka kwamba chochote... Bali akiwa asiye na kikomo ingembidi kujua. Kwa hiyo, basi, Yeye angeweza kusema ya kwamba atakuwa na Kanisa lisilo na waa wala kunyanzi, kwa sababu alijua Yeye atakuwa nalo. Yeye ni Mungu.

114 Sasa, na mahali hapa pa kupendeza katika bustani ya Edeni, loo, ambako wanaume na wanawake waliishi pamoja. Mungu ni mkandarasi mkuu.

115 Sasa, mna wengi wa hao hapa Tucson, panavyoendelea kujengwa. Miaka michache iliyopita, nilipokuwa hapa, jiji dogo tu. Na sasa, kule juu ninakoishi, mbona, koyote na Papago walikuwa wakipitia kule nilipokuwa hapa miaka michache iliyopita. Na sasa kuna... Mbona, ni miradi mikubwa, na nyumba, na kuendelea kujenga zaidi, zaidi, zaidi, zaidi. Vema, ni nini kinachoendelea? Mnaona, makondrakta huingia na kununua kipande cha ardhi, na kukigawanya, na kujenga nyumba.

116 Sasa, Mungu alifanya hivyo. Mnaona? A—aliweka nyenzo zote, kuifanya miili yetu, wakati ulimwengu huu ulipokuwa unaumbwa. Sasa, tumeumbwa kwa elementi kumi na sita, hizo ni chumvi, na kalisi, na petroli, na nurulimwengu, na kadhalika.

Na hizi zote zinajumuika pamoja kumfanya mtu. Lakini hiyo ilikuwa hapa kabla hapajakuwapo na mtu duniani. Mnaona? Mungu aliiumba miili yetu na kuziweka nyenzo hapa nje kabla hapajakuwapo na dunia.

¹¹⁷ Sasa, unaingizwa ndani yake na unakuja hapa kwa njia ya Mungu. Na sasa unayo nafasi ya kuishi Milele kama ukichagua hivyo. Hiyo ndiyo hasa Adamu na Hawa waliyokuwa nayo. Kila... Mungu hawezi kubadilika. Hana budi kubaki vile vile, ampe kila mtu nafasi ile ile.

¹¹⁸ Sasa tunaona, Mungu, ilimpendeza wakati alipomwumba mwanadamu. Aliangalia nanii Wake—binti Yake na mwana Wake, na jinsi Yeye alivyopendeza nao. Ndipo basi tunakuta kwamba, punde tu Adamu na Hawa walipokuwa wametenda dhambi, na ujumbe huo ukaja mbele za Mungu, Baba yetu, “Mtoto wako ameanguka kutoka kwa neema. Amekuondokea Wewe.” Jamani, jinsi hilo hapana budi liliushtusha moyo Wake!

¹¹⁹ Na sasa angalia tabia hiyo. Hapo Adamu alipotambua ya kwamba alikuwa amepotea, wakati alipojua ya kwamba alikuwa amefanya kosa na ikadhihirishwa mbele zake, kwamba alikuwa makosani. Badala ya kuita, “Ee Baba, njoo kwangu; nimepotea; nimekosea; nimedanganyika; njoo kwangu,” yeye alijificha.

¹²⁰ Basi ilikuwa ni Mungu, akienda huku na huku bustanini, akipiga mayowe, “Adamu, uko wapi?”

¹²¹ Hivyo si ndivyo ilivyo leo hii? Unaweza ukawaonyesha watu, kwa Neno la Mungu, wakati ameshindwa. Hiyo ni hakika. Adamu alijua alikuwa ameshindwa. Alikuwa amelikosea Neno la Mungu.

¹²² Nanyi kumbukeni, haihitaji mengi sana. Mnajua ni kitu gani kilichosababisha maradhi haya yote, na shida hii yote, na mauti, na huzuni, ya miaka elfu sita? Kwa sababu mwanamke mmoja alishindwa tu kuamini fani moja ndogo, fungu moja dogo la Neno la Mungu, chembe moja tu ndogo. Aliamini karibu lote. Shetani alimwambia Ukweli wa karibu Hilo lote. “Mambo haya utafanya, na *hili*.” Na kisha akasema, “Hakika hamtakufa.”

¹²³ Lakini kutokuamini tu chembe moja ndogo, kulisababisha shida hii yote. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mnafikiri kutokuamini chembe moja kutawarudisha, baada ya kusababisha hayo yote? [“La.”] La, bwana.

¹²⁴ Hatuna budi kuja kwenye Neno. Hilo tu ndilo, na Hilo ni Mungu. “Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.”

¹²⁵ Basi, mnaona, Mungu alipomwumba mwanadamu, wakati alipoanza kuiatamia dunia, yakatokea, kama maua ya Pasaka, nyasi zikatokea, spishi zikatokea, zikiinuka juu zaidi na zaidi. Roho Mtakatifu mkuu, akiatamia! Ama, *kuatamia* kunamaanisha “kulea, kuita kwa upendo.” “Kuu, kuu.” Maua

yakachomoza. Baba akasema, “Hayo ni mazuri sana. Endeleeni tu.” Ndipo Yeye akaatamia. Basi baada ya kitambo kidogo, wakaja ndege. Na kilichofuata, wanyama wanatokea. Aliendelea kuwa mkubwa zaidi, mkubwa zaidi, mkubwa zaidi, mkubwa zaidi.

¹²⁶ Ndipo, hatimaye, dunia ikaakisi uakisi Wake aliyekuwa akiatamia: Mungu. Naye alikuwa katika mfano wa Mungu. Kamwe hakuna kitu kilichotokea cha juu kuliko mwanamume, hata kwa dada zetu wapendwa, mwanamke. Yeye hayuko katika uumbaji wa asili. Yeye alitokana na mwanamume, sehemu yake; nao ni mmoja, katika Kristo. Loo, ni somo kubwa jinsi gani tulilo nalo hapa moja kwa moja mbele zetu sasa, ambalo tungetumia saa kadhaa juu yake, kulifafanua! Angalieni.

¹²⁷ Sasa tunaona ya kwamba, basi, wakati mtu huyu alipomwakisi Mungu, ndipo Mungu aliposhuka katika uakisi Wake mwenyewe, katika mfano wa Mwanadamu, Yesu Kristo. Naye Mungu alikuwa ndani ya Kristo. Yule Mungu, ndani ya Kristo, akijiakisi Mwenyewe kwa dunia, kile Yeye alichokuwa: Mwokozi, Mungu, Mponyaji. Mungu, akionyesha sifa Zake halisi, kupitia Mtu, ambaye alikuwa ni uakisi Wake. Naye Mungu, kusudi apate hili, asingeweza kuja kupitia kujuana kimwili, ambalo ndilo chanzo cha mambo yote, lakini alilileta kupitia kwa kuzaliwa na bikira.

¹²⁸ Hivi hamwezi kuona hiyo, hiyo dhambi ya kwanza, kwamba ilikuwa ni kitu gani? Wengi hawatakubaliana na hilo, nanyi mnapayuka-payuka kuhusu “ule uzao wa nyoka,” lakini hiyo hapo. Mnaona?

¹²⁹ Sasa, uakisi, Mungu akijiakisi Mwenyewe ndani ya Kristo. Lakini basi wakati mtu huyu alipopotea . . .

¹³⁰ Leo hii, wakati mtu anapoonyeshwa, kwa Neno, kwamba hapaswi kufanya mambo haya, wakati mwingine yeye ni mwaminifu kwa kanisa.

¹³¹ Kama kuna yeyote wa marafiki zangu Wakatoliki hapa asubuhi ya leo, samahani hili kwa dakika moja tu. Watu wangu wote ni Wakatoliki pia, mwajua, Katoliki ya Kirumi.

¹³² Sasa angalieni. Wakati kasisi huyu aliponijia, kuhusu uponyaji mwingi mkuu, naye akasema, “Msingi wako ni Katoliki. Kwa nini wewe si Mkatoliki?”

Nikasema, “Mimi ni mkatoliki.”

Naye akasema, “Loo, siwezi kuamini hilo.”

¹³³ Nikasema, “Hivi kanisa lenu halifundishi ya kwamba Biblia hii, ya kwamba Yesu Kristo alianzisha kanisa katoliki la kwanza, na hawa mitume walikuwa wakatoliki?”

“Naam.”

Nikasema, “Basi mimi ninaamini kile tu walichoandika.”

¹³⁴ Akasema, “Lakini, Bw. Branham,” kasema, “kanisa linaendelea kubadilika. Yeye alimpa Petro mamlaka ku—kuwa na zile funguo, naye anaweza kufunga, na urithi wa kimitume wa mapapa, na kadhalika.”

¹³⁵ Nikasema, “Ninayo maandishi yenu yote, ama karibu yote, mle ndani, *Kweli Za Imani Yetu*, na kadhalika. Lakini,” nikasema, “angalia. Kama wale watu walioandika Biblia hiyo, walitembea kwa pamoja na Yesu, unasema walikuwa ni katoliki nao wakaiandika ile Biblia, hivi hufikiri wangejua zaidi juu ya mapenzi ya Mungu, na amri za Mungu, kuliko vile kundi hili mambo leo lingejua leo hii?” Tena nikasema, “Angalia, kama ni Kanisa, basi wakati walipotii yale Mungu aliyosema, awali, na ni Neno la Mungu, angalia ile miujiza na ishara, na kadhalika, walizokuwa nazo. Nanyi hamnazo hata kidogo, leo hii. Ni ushahidi kwamba Mungu hayuko pamoja nanyi.”

Akasema, “Bw. Branham, hatupaswi kubishana.”

¹³⁶ Nikasema, “Bwana, nisingebishana na mtu yeyote. Ninakuuliza tu jambo fulani.” Kisha nikaleta lile Baraza la Nikea na kadhalika.

¹³⁷ Akasema, “Hatupaswi kubishana.” Akasema, “Unajaribu kuzungumza juu ya Biblia, juu ya Neno.” Kasema, “Mungu yuko katika kanisa Lake. Hivyo ndivyo kanisa *lilivyokuwa*. Hivi ndivyo lilivyo leo hii. Tunapaswa kulisikiliza kanisa leo hii.”

Nikasema, “Mungu yuko ndani ya Neno Lake.”

Akasema, “Mungu yuko katika kanisa Lake.”

¹³⁸ Nikasema, “Yeye yuko katika Neno Lake. Na ikiwa Neno haliko ndani ya kanisa, basi Mungu hayuko ndani ya kanisa, kwa sababu Neno ni Mungu.” Kisha nikasema, “Isitoshe, je! unaamini kitabu cha Ufunuo?” Ambalo linamaanisha, “Funuo.” Ni Kiyunani. “Unaamini kitabu cha Ufunuo kimevuviwa?”

Kasema, “Hakika.”

¹³⁹ Nikasema, “Basi, Yesu Kristo alisema, Mwenyewe, katika Ufunuo, ya kwamba, ‘Yeyote atakayeondoa Neno moja kutoka Kwake, au kuongeza neno moja Kwake, sehemu yake itaondolewa kutoka kwenye Kitabu cha Uzima.’ Basi wawezaje kusema ya kwamba una mamlaka ya kuondoa, kuingiza, ama kufanya utakacho, wakati umekatazwa kufanya hivyo na mwanzilishi wa Kanisa la Kikristo, Yesu Kristo? Huwezi kufanya hivyo.” Mnaona?

¹⁴⁰ Loo, ile saa, ule wakati wa ajabu sana tunaoishi! Na wakati watu wanapoambiwa kuhusu kosa lao, badala ya kujaribu kurudi na kusema, “Baba, nimekosea; nisamehe,” wangali wanajificha nyuma ya majani ya mtini. Majani ya mtini ndiyo waliyojishonea, wenyewe. Nao wakajaribu ku... Neno *dini* linamaanisha “kifuniko.” Nao walijaribu kujitengenezea

kifuniko cha kutengenezwa kwa mkono. Na mwanadamu hajabadilika bado, leo hii.

¹⁴¹ Kwa hiyo, Mungu ilibidi aitische kongamano. Na ilibidi Yeye akutane na mtu Wake, mtoto Wake.

¹⁴² Basi kumbukeni, amri Zake zilikuwa, “Siku utakayokula kwenye huo, siku hiyo utakufa.” Na Mungu hawezi kuzigeuka amri Zake mwenyewe na awe mwenye haki. Kwa hiyo aliweka shimo kubwa kati Yake na mwanadamu. Kwa hiyo wakati wao. . .

¹⁴³ Yeye alitaka kumkomboa mtoto Wake. Hakutaka waende namna hiyo, kwa hiyo ilimbidi Yeye kumkomboa. Kwa hiyo waliitisha kongamano, na lilikuwa ndilo kongamano la kwanza ambalo Mungu aliwahi kukutana na mwanadamu, lilikuwa ni lile kongamano la Edeni.

¹⁴⁴ Yeye atamwokoaje mtu huyo? Anaweza kufanya nini, ili kuwarudisha Kwake watoto Wake waliopotea? Pia kumbukeni, uamuzi Wake wa kwanza ni mkamilifu, daima.

¹⁴⁵ Kama ingalikuwa ni kanuni za imani, majani ya mtini, Yeye angalisema, “Adamu, umefanya haki. Toka nyuma ya miti. Nafikiri wewe ni mtu mwenye hekima. Unaniakisi Mimi, kwa sababu wewe ni mwenye hekima. Majani yako ya mtini ni mazuri tu.” Mwanadamu angali anajaribu hilo jani la mtini.

¹⁴⁶ Lakini Mungu alifanya uamuzi. Nao uamuzi huo ulikuwa, kwamba, kitu fulani ilibidi kife, kwa sababu kilinena juu Yake, utakatifu Wake na haki, kwa Sheria Yake Mwenyewe. “Siku utakayokula kwenye huo, utakufa.” Basi ilibidi pawe na kibadala chenye hisi. Uhai wa mimea hauna hisi. Kwa hiyo ilimbidi Yeye kuua kitu fulani kusudi apate ngozi, kuwafunika. Na huo ulikuwa ndio uamuzi wa Mungu, jinsi ya kumwokoia mwanadamu, kumrudisha mwanadamu katika ushirika na Yeye, huko Edeni, na daima imebaki hivyo. Hakuna mtu. . .

¹⁴⁷ Sijui ni mara ngapi ambapo wamejaribu kumwelimisha mwanadamu. Wamejaribu kumwambia ya kwamba mpango wa elimu utatosha. Ni mara ngapi makanisa yemejaribu hiyo? Imeshindwa kila wakati, na itashindwa. Tunajaribu kuunda dhehebu, kila jamaa analo. . . Sasa, mimi sipingi elimu, wala sipingi dhehebu. Lakini mipango ya kidhehebu na ya kielimu, na yote mengine ambayo tumejitengenezea, ni majani ya mtini.

¹⁴⁸ Ni, kurudi kwenye uamuzi asili wa Mungu kwenye lile kongamano la kwanza, Edeni, kurudi kwenye damu! Myahudi, zamani za kale. . .

Sasa ninashuka kuja nyumbani, kwa Pentekoste, kwa dakika chache tu.

¹⁴⁹ Zamani za kale, wakati Mungu alipokubali kibadala hiki, jinsi Myahudi alivyokuwa akishuka kuja barabarani pamoja na fahali wake laini. Naye angesema, “Unajua, mimi ni

mwenye dhambi. Yehova ananitaka nitoe damu.” Kwa hiyo anaenda na kuchukua mwana-kondoo wake ama fahali wake. Anampeleka huko chini kwa kuhani mkuu, huko hekaluni, ndipo anaweka mikono yake juu ya dhabihu yake. Hilo linafanya nini? Hilo humtambulisha mwabudu na dhabihu yake. Basi kuhani anakuja na kumwua huyo fahali, kisha anaichota damu na kuinyunyiza juu yake. Naye huyu mwabudu akijua kwa uaminifu, huyu Myahudi, ya kwamba hiyo ndiyo Yehova aliyohitaji kwake.

¹⁵⁰ Mtu huyo alienda nyumbani akijisikia vizuri, akiuhisi mtetemo na kutetemeka kwa mwana-kondoo huyo, damu ikirashia mikono yake yote, na kadhalika, na kumwona maskini jamaa huyo akirusha mateke na akifa, huku shingo yake ikikatwa. Alijua ya kwamba alipaswa kuwa huyo. Aliangalia dhabihu yake. Alijitambulisha mwenyewe kwa kuiweka mikono yake juu yake, “Ninapaswa kuwa huyo.” Ndipo basi walipoikata shingo yake, yeye akifa na kulia, na kupiga makelele, na maskini jamaa huyo anatetemeka na kuanza kutulia, naye mwabudu anasimama pale na kusema, “Ee Yehova, umemkubali huyo badala yangu. Ninajionea aibu.” Basi mtu huyo akaenda nyumbani amehesabiwa haki, kwa sababu alikuwa amefanya yale hasa Yehovah aliyohitaji. Hilo lilikuwa sawa.

¹⁵¹ Lakini, muda si muda, ikawa ni desturi ya familia. Sasa yeye anaichukua dhabihu yake, kasema, “Vema, hebu tuone, sasa. Loo, naam, inaelekea mwezi mwandamo, karamu. Nadhani ni afadhali. Ni utakaso, maskanini. Ni sikukuu ya pentekoste. Nadhani ni afadhali nishuke niende, nikajitolee mwana-kondoo.” Anashuka anaenda kule na kumchinja, pasipo na hisi hata kidogo; bali anarudi na wazo lile lile alilokuwa nalo, akija mle.

¹⁵² Ndipo basi Yeye alifanya nini? Yehova alisema, hapa katika Isaya, akizungumza baadaye kidogo, Alisema, “Sikukuu zenu zilizoamriwa zimekuwa uvundo puani Mwangu.” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹⁵³ Hatuna budi kuja, sio kama kundi la akina riki na riketa. Hatuna budi kuja, sio kama kundi la kawaida, ama kadhalika, walilo nalo leo hii, la dini hizi za mapokeo. Sisi ni wapentekoste. Hebu tuje na uaminifu wa kilindi, tuiweke mikono yetu juu ya Dhabihu yetu huko Kalvari, na kuhisi kule kutokwa na damu na mateso ya Yesu Kristo, wakati tukijitambulisha wenyewe kwamba tumekufa kwa mambo ya ulimwengu na mawazo haya mamboleo ya siku hizi.

¹⁵⁴ Tuko kama Sodoma na Gomora, nasi tunaishi katika hiyo. Hebu na roho yenye haki iliyo ndani yetu... Dhambi hizi zinachukiza nafsi yetu kila siku; hebu dhambi za ulimwengu, na mitindo ya Hollywood, na uinjilisti huu wote wa Hollywood

na upuuzi, kujipodoa huku kote, na kupiga muziki, na kurukaruka. Muziki ukikoma, wewe huyo unashuka.

¹⁵⁵ Wakati mtu ameoshwa katika Damu ya Mwana-Kondoo, hahitaji muziki wala chochote kingine. Nguvu za Mungu zinatenda tu kazi juu yake, naye anaweza kupaza sauti, kupiga makelele, kumsifu Mungu, ama kufanya chochote kingine, kuwe kuna muziki ama hakuna. Roho Mtakatifu yuko ndani yake, naye ametambulishwa na Yesu Kristo.

¹⁵⁶ Lakini, leo hii, tunataka tu kufanya hivyo. Hatuna budi kuruka-ruka kidogo, kama Wapentekoste, maana babu zetu walifanya hivyo. Wao walikuwa na jambo la kuruka-rukia, huyu Roho Mtakatifu akiwafanya waruke. Ndipo basi waliposhuka chini, daima ishi kadiri ulivyoruka juu. Kama sivyo, usiruke hata kidogo. Tunashuka leo hii na kuishi kila namna za maisha. Tunaleta uakisi juu ya Jambo lile lile tunalotetea.

¹⁵⁷ Nayo madhehebu yetu yanaanza kuwa ya kilimwengu. Wanatoka kule nje na kuwaacha ndugu zetu wa Kipentekoste kwenda huko nje katika shule hizi mashuhuri. Hayo ni sawa, hamna neno dhidi yake, bali ninajaribu tu kuonyesha hoja fulani. Wanawaelimisha, na kuwafundisha saikolojia, na kuwapa B.A. na kama tu vile hao wengine wafanyavyo, na kuwatuma huko nje. Na kile walicho, hao kabisa... Hao si pentekoste.

¹⁵⁸ Mungu hana wajukuu wowote. Mungu anao wana. Tunajaribu kufikiri mama yetu alikuwa mpentekoste, na baba yetu alikuwa mpentekoste, na sisi sote tulilelewa katika shule ya Jumapili, basi moja kwa moja sisi ni wapentekoste. Hao ni wajukuu. Mungu hana wajukuu.

¹⁵⁹ Yeye anao wana wa Mungu na binti za Mungu, na kila mtu hana budi kulipa gharama ile ile aliyolipa mtu wa kwanza. Hana budi kuja chini ya Damu iliyomwagika ya Yesu Kristo. Hivyo ndivyo hana budi kufanya. Sasa tunaona, sasa, ya kwamba hivyo ndivyo, hapo mwanzo, ule uaminifu.

¹⁶⁰ Sasa tunajaribu kuwazia, kwa sababu tunaye jamaa mdogo hapa ambaye anataka elimu, yeye anaenda huko nje shuleni na kadhalika, anatokea akiwa ameelimika. Anaweza kuzungumza kwa njia ya kupendeza mno. Anaweza kusimama jukwaani. Yeye ni mtu wa madoido. Vema, hiyo ni Hollywood. Wanataka kitu kinachong'aa. Mnataka mtu mwenye utamaduni, pamoja na elimu nzuri. Mnamtaka mtu, haidhuru, aliye na mawazo mapana, ambaye anaweza kuona hajali wanawake kukata nywele zao. Biblia ilisema yeye asizikate. Hajali ninii... Kama shemasi akiya kanisani, kama ni mtu mzuri na anaweza kulipa vizuri sana, hawajali kama ameo mara kadhaa. "Hilo ni sawa. Yeye ni jamaa mzuri." Lakini Biblia inalikataa hilo. Kabisa.

¹⁶¹ Hatuingii kanisani kwa theolojia. Tunaingia kwa elimu ya magotini. Hiyo ni kweli. Tunaingia ndani ya Kristo.

¹⁶² Lakini, mnaona, leo hii tuna—tuna wazo hili ya kwamba tunataka kwenda kama hao wengine. Hilo ndilo lililowaingiza Israeli taabuni, walitaka kwenda kama hao wengine. Sikukuu yetu yenye uchaji ya pentekoste imekuwa ni ibada ya kawaida tu. Sote tunajua hilo. Nasi tunalionga likianza . . . Haitupasi kufanya hivyo.

¹⁶³ Jambo ambalo hatuna budi kufanya ni kurudi na kujitambulisha wenyewe na Yesu Kristo. Tuchukue njia Yake na tumwache Yeye atende kazi kupitia sisi, ndipo watu watamfuata kwa furaha Yeye ambaye wakati mmoja alifundisha, “Nitawavuta watu wote Kwangu.”

¹⁶⁴ Jinsi tungalitaka kuendelea kidogo, na kuelezea jambo lingine zaidi juu ya kongamano hilo la Edeni, bali nina kongamano jingine zaidi ninalotaka kuendea.

¹⁶⁵ Kwa mfano, hebu tupate kongamano lingine: Kongamano la Kichaka Kilichowaka Moto, ningeliita, Kichaka Kilichowaka Moto.

¹⁶⁶ Sasa, Mungu alikuwa na nabii mtoro. Mungu anapomwita mtu kufanya jambo fulani, ni heri tu alijie, ama atakuwa na taabu siku zake zote. Musa alianza. Aliitwa na Mungu. Alichaguliwa kufanya kazi fulani. Ndipo basi wakati alipoanza, watu hawakumwamini, kwa hiyo aliwaacha tu watu waende. Alitoroka na kumwoa msichana mrembo wa Ethiopia, na kupata urithi, akarithi kundi la kondoo. Naye huyo hapo, huko nje, naye alipoteza ono lote la hao watu, la kanisa la Mungu aliye hai. Naye Mungu alikuwa amemchagua kuifanya. Alimwinua, “alizaliwa kutoka kwenye tumbo la mama yake, mtoto mzuri,” na Yeye akamkuza kwa kusudi hili. Hakuna haja ya kujaribu kulitoroka, utalifanya, haidhuru.

¹⁶⁷ Na nyinyi, wafuasi wa kanisa tu, nawe unajisikia ya kwamba kuna kitu fulani chenye kilindi zaidi moyoni mwako, utakuwa maskini mwenye mashaka mpaka utakapomkubali huyo Kristo, namna hiyo. Umemwona Roho Mtakatifu halisi akifanya kazi ndani ya watu. Utakuwa mwenye mashaka mpaka atakapokuja kwako. Ni Mungu akikuia. Jisalimishe. Toka nje, nyuma ya vichaka. Imetatuliwa tayari. Mungu alifanya njia Yake. Ni kupitia kwa Damu.

¹⁶⁸ Unasema, “Vema, mimi ni mshiriki wa kanisa.” Hilo halimaanishi kidogo zaidi ya kama ulikuwa shabiki wa mashindano ya wachunga ng’ombe, si hata kidogo. Sina neno dhidi ya dhehebu; lakini siwapingi watu katika dhehebu, bali ni huo mfumo.

¹⁶⁹ Sasa angalieni hili. Sasa tunakiona kichaka hiki kinachowaka moto. Mungu alijua ya kwamba nabii huyo alikuwa akiishi raha mstarehe, kwa hiyo Yeye aliamua kwamba itambidi Yeye kuzungumza na nabii huyu. Kwa hiyo, Yeye akachagua mahali fulani. Hali ya dharura ilikuwa imeingia,

“Nimesikia kilio cha watu Wangu. Na kuna mtu niliyemtuma akawakomboa, naye ni mnyonge na dhaifu.”

¹⁷⁰ Ee Mungu, natumaini atamwita mmoja hapa asubuhi ya leo, wahudumu wapate moto. Waangalie lile ono. Tunakufa. Ulimwengu umekwisha. Kanisa limerudi nyuma. Mungu anajaribu kuita Bibi-arusi atoke.

¹⁷¹ Kwa hiyo, Yeye alichagua mahali, mahali pa kipekee sana kwetu; palikuwa ni kichaka juu ya mlima. Lakini hicho kilivutia usikivu wa nabii. Na Yeye akamwita kule juu kwa ajili ya kongamano.

¹⁷² Angalia. Ilimbidi kutii, neno kwa neno. “Vua viatu vyako, Musa. Mahali unaposimama ni patakatifu.”

¹⁷³ Vipi kama Musa angalisema, “Vema, sasa, Bwana, ndio kwanza nipate mafunzo fulani. *Heshima* ni ‘toa kofia yako,’ kwa hiyo nitatoa kofia yangu”? Hilo lisingefanya kazi.

Mungu aliposema, “Viatu,” Yeye alimaanisha viatu.

¹⁷⁴ Mungu aliposema, “Kuzaliwa mara ya pili,” Yeye alimaanisha kuzaliwa mara ya pili. Hamaanishi kupeana mkono ama kurudia kanuni ya imani. Kila mtu anaogopa huko Kuzaliwa upya.

¹⁷⁵ Ibilisi aliweka kupeana mikono badala Yake, ama namna fulani ya jambo la kiakili, ambalo lingekufanya ukubali, “Naam, nimezaliwa mara ya pili.” Bali maisha yako yanaonyesha kwamba wewe ni nani, uhai ulioko ndani yako.

¹⁷⁶ Unasema umezaliwa kwa Roho wa Mungu, na kukana Neno moja la Biblia hiyo, inaonyesha kwamba hujazaliwa. Unajaribu kuliweka Hilo huko nyuma kwa kitu kingine, hiyo inaonyesha haikuwa ni Roho Mtakatifu, maana Yeye kamwe asingelikana Neno Lake Mwenyewe. Unasema, “Vema, kanisa langu linafundisha *hilo*.” Hapo, inaonyesha sivyo ulivyo. Umezaliwa na kanisa, sio na Mungu. *Hili* ni Mungu, Neno Lake.

¹⁷⁷ Huyu hapa, Musa, aliyepakwa mafuta. “Vua viatu vyako. Umesimama mahali patakatifu.”

¹⁷⁸ “Vema, hivi si kofia yangu itafaa vivyo hivyo?” Yeye alisema viatu. Na hivyo ndivyo Yeye alivyomaanisha, ilikuwa ni viatu.

Mungu anasema, “Uzaliwe mara ya pili.” Inamaanisha kuzaliwa mara ya pili.

¹⁷⁹ Sasa sikilizeni. Loo, niko kwenye umati uliochanganyikana, na watoto wadogo. Lakini mngemsikiliza daktari wenu. Sikilizeni. Natumaini mtanisikiliza na kuelewa.

¹⁸⁰ Kuzaliwa kwokwote ni mchafuko. Sijali kama ni katika kizimba cha nguruwe, ama—ama ni katika chumba kilichopambwa waridi cha hospitali. Mchafuko wowote... kuzaliwa ni mchafuko. Vivyo hivyo na kuzaliwa Upya. Ni mchafuko. Kutakufanya ufanye mambo hukuwazia

ungeyafanya. Lakini kutokana na huko kufa na kuoza unakuja Uzima.

¹⁸¹ Na hakuna mbegu inayoweza kuleta uhai wake isipokuwa imekufa na kuoza. Na kutoka kwenye uchafu huo uliooza, wakati hakuna kingine kilichosalia kuuoza, uhai tu ndio unaoishi. Mwana anapomjia Mungu, yeye anapewa majaribu.

¹⁸² Nilisimama pale siku hiyo, ninakumbuka, wakati nilipojaribiwa. Wakati nilipokuwa siku baada ya siku, miezi baada ya miezi, na miaka, miaka minne au mitano mitaani, pembeni, nikihubiri Injili, na kujaribu kufanya yale yaliyokuwa sahihi machoni pa Mungu. Naye akamwacha mke wangu kuondoka moja kwa moja chini yangu. Mtoto wangu mchanga amelala pale, akifa. Ndipo nikashuka nikamwendea mtoto huyo mchanga, nikasema, “Bwana Mungu, usiache mtoto wangu mchanga afe,” umri wa miezi minane, tisa, mtoto mchanga.

¹⁸³ Nikainua macho yangu, na ilionekana kana kwamba shuka jeusi linashuka. Hata alikataa kunisikia. Hata asingeniangalia. Nikasimama, yapata umri wa miaka ishirini na mitatu. Huyo hapo mke wangu amelala kwenye chumba cha maiti. Yeye alikataa kunisikia, kwa ajili yake, wakati yote niliyokuwa nimefanya. Nikasema, “Mungu, niambie nimefanya nini. Kama nimefanya makosa, niadhibu mimi, sio wao.” Nikasema, “Nimefanya nini? Kufanya kazi siku nzima, na kuhubiri usiku kucha, na kusimama pembeni mwa barabara. Na kila... Nimefanya nini? Niambie kile nimefanya?” Hata hangeniambia.

¹⁸⁴ Ndipo Shetani akaja karibu nami. Akasema, “Halafu utamtumikia Yeye, wakati neno moja lingebadilisha hali yote? Neno moja litamwoko mtoto wako mchanga, lakini Yeye anakataa kumwoko. Hatamwoko; wakati neno moja. Halafu utaondoka uende ukamtumikie Yeye?”

¹⁸⁵ Hoja zote za kibinadamu, hiyo ni kweli. “Kwa nini nimtumikie kama hata hataangalia chini kwenye mtoto wangu mchanga, na hilo lingelitaji yote yanayohitajika? Na kadiri nilivyowazia nimemfanyia Yeye, halafu Yeye hata hatamsikia mtoto wangu mchanga.” Hilo lilikuwa ndilo jaribu gumu kuliko yote. Hoja zote za kibinadamu zilikuwa zimevurugika. “Kwa nini nimtumikie Yeye kama Yeye hawezi kunitendea kiasi hicho? Nami ninaenda mchana na usiku, kwa ajili Yake, na Yeye hata anakataa kuniambia yale niliyofanya.” Vema, hoja za kibinadamu zimekwisha.

¹⁸⁶ Lakini, loo, wakati mtu amezaliwa mara ya pili, hicho ni kitu mle ndani kinachoshikilia. Ikashuka kufikia mahali hapo, wakati nilipowazia, “Hivi nilimpata wapi? Alitoka wapi? Mimi ni kitu gani, hata hivyo? Nilitoka wapi?” Mnaona? Sehemu zote za kibinadamu zilikuwa zimepasuka, ndipo yule Roho halisi wa Mungu akakaa pale.

¹⁸⁷ Nikajongea kwake na kuweka mikono yangu juu ya kichwa chake. Alikuwa anateseka sana hata macho yake madogo yalikuwa yakiingia mkengeza. Nikasema, “Kipenzi, katika dakika chache, nitakuchukua na kukuweka mikononi mwa mama, huko nje kwenye—kwenye chumba cha maiti. Nitakuzika hapa nje chini ya misonobari. Na siku moja baba atakuona tena.”

¹⁸⁸ Nikainua macho yangu. Nikasema, “Mungu, ingawa Wewe utaniua, hata hivyo nitakutumaini Wewe. Ulinipa huyu. Umemchukua. Jina la Bwana libarikiwe.”

¹⁸⁹ Kwa kuwa, wakati huo, hoja zangu zote za kibinadamu zilikuwa zimetoweka. Nilikuwa nimefikia mwisho wa safari yangu. Lakini unapofikia mwisho wa safari yako, basi kuna yule Roho halisi wa Mungu hapo kushika usukani, wakati huo, na kukuinua.

¹⁹⁰ Huna budi kuzaliwa mara ya pili. Kila kitu hakina budi kufa. Theolojia yako yote, mawazo yako yote, yote uliyowahi kuwa ama unayotarajia kuwa, maisha yako na kila kitu kingine, vinakufa. Ndipo Roho Mtakatifu anaingia. Hapo ndipo unapovua kofia, viatu, unasimama mbele za Mungu. “Sina cha mkononi ninacholeta. Ninajishikilia tu msalabani Pako.”

¹⁹¹ Hapo ndipo ilimbidi Musa kuja, ambapo angeweza kutii yale Mungu aliyosema afanye; lile Kongamano la Kichaka Kilichowaka Moto. Ndipo Mungu akasema, “Nitakuonyesha utukufu Wangu sasa,” akiisha kuwa radhi kwenda. Ndipo akashuka akaenda Misri.

¹⁹² Hilo hapo kongamano la Edeni. Hilo hapo Kongamano la Kichaka Kilichowaka Moto.

¹⁹³ Hebu tuchukue lingine, upesi sana. Hebu tuchukue kongamano la Bahari ya Shamu. Mnajua, moja kwa moja kwenye wajibu, wakati mwingine, Shetani hupita njiani mwetu. Ndugu wahudumu, nyote mnajua hilo. Enyi Wakristo, mnajua hilo. Kweli.

¹⁹⁴ Huyu hapa Musa, akishuka kwenda, na akawaonyesha Israeli ishara; wale aliowaonyesha ya kwanza, nao wasingesikiliza. Yeye anarudi kwenye wajibu, chini ya upako wa Mungu, akiwa na sauti yenyewe ya Mungu ya kunena vitu hata vikawepo. Angeweza kuwaita nzi. Alitumia sauti ya Mungu. Akasema, “Nzi na waje.” Na hapakuwapo hata na nzi nchini. Akarudi nyuma. Alijua litatukia kwa sababu alikuwa amenena Neno la Mungu. Akarudi nyuma. Ndipo moja kwa moja maskini nzi wa kijani akaanza kuzunguka-zunguka, na kisha wakawa pauni mbili kwa yadi moja mraba.

¹⁹⁵ Kazi ya uumbaji, hiyo ni mali ya kanisa la Yesu Kristo leo hii, chini ya Damu ya Yesu Kristo, kwa Neno Lake, kwamba tuna mawasiliano na Yeye. Hakuna tofauti. Neno tunalosikia lipo hapa, nalo ni Mungu. Tunamwona akisimama pale. Tunajua

ni Yeye akituzungumzia, jambo lile lile. Nimeliona likifanywa, nami ninajua ni kweli. Liko pamoja na Biblia.

¹⁹⁶ Hapo, Musa, amepewa mamlaka. Akashuka akaenda na kuwaonyesha Israeli ishara, nao Israeli wakatoka pamoja naye. Nao hawa hapa, moja kwa moja kwenye wajibu, na ile pale Bahari ya Shamu ikiwazuia. Musa aliitisha kongomano. Hapana shaka Mungu alichagua mahali fulani nyuma ya Mwamba. Musa anaenda kule, na kusema, “Bwana!”

¹⁹⁷ Kama unatembea kwenye wajibu, una haki ya kuitisha kongamano. Hilo ndilo tumekuja kuombea. Hilo ndilo linalofanya tutumwe hospitalini. Hiyo ndiyo sababu tunaenda kwenye kitanda cha wagonjwa. Kuitisha kongamano. Loo, jamani! Ninajisikia wa kidini sasa hivi. Itisha kongamano. Hilo ndilo Wapentekoste wanalohitaji leo hii, ni kuitisha kongomano. Kuna shida gani? Tulipunguza mwendo. Kuna kabari kambini mahali fulani. Itisha kongamano.

¹⁹⁸ Musa aliitisha kongamano, kasema, “Bwana, nimefanya jinsi hasa Wewe ulivyoniambia, na sisi hawa hapa katika mtego. Mauti yanakuja, yanatujongelea.” Kama mgonjwa mwenye kansa, “Mauti yanatujongelea.” Basi Musa akasimama pale mpaka wakafanya mazungumzo na Mungu. Alikaa pale mpaka Mungu akanena. Alijua sauti Yake. Yeye alikuwa ni nabii.

¹⁹⁹ Kasema, “Kwa nini unanililia Mimi, Musa? Nilikupa mamlaka kuwapeleka watu hao kule, na nikakwambia utawapeleka. Nena na watu na msonge mbele.” Amina. Bahari ya Shamu ikaanza kusogea, na kila kitu kingine, wakati Mungu aliponena Neno. Wakati uamuzi ulipokuja kwa ajili ya kile anachopaswa kufanya.

“Nipo hapa. Ninakabiliana nayo. Nifanye nini?”

“Nena na usonge mbele.” Nayo Bahari ya Chumvi ikasogea.

²⁰⁰ Wakati wetu unaisha. Na ni—nina mengi sana, mahali mbalimbali, ninapotaka kurejea. Na tuharakishe. Nina wengine kadhaa, Daudi, na kadhalika.

²⁰¹ Lakini hapa, kumbukeni, kulikuja kongamano la Gethsemane wakati mmoja, wakati ilipombidi Mungu na Mwana Wake kukutana. Hata hivyo, hapakuwapo na mwingine angaliweza kufa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu. Hapakuwapo na mtu aliyestahili kufa, hakuna mtu.

²⁰² Kila mtu katika ulimwengu huu alizaliwa kwa tamaa ya kujuana kimwili, na hilo ndilo lililosababisha ule mchafuko pale mwanzo. Hilo ndilo lililoyasababisha, likatufanya viumbe chotara. Tumezaliwa kwa kujuana kimwili, tamaa ya kibinadamu. Ni uchotara. Kitu fulani kimekuwa...Hiyo ndiyo sababu kina mauti ndani yake, kama nilivyozungumzia jana usiku. Lakini hapo Mungu alipomfanya mwanadamu Wake wa kwanza, kamwe hakumwagiza mwanamke na mwanamume

kuja pamoja. Yeye alimuumba kutoka ardhini. Alikuwa ni mmea halisi. Dhambi yake ndiyo iliyomleta kwenye uchotara.

203 Hiyo ndiyo shida leo hii, sababu ya sisi kupata Wapentekoste wengi sana machotara. Mnasikiliza hoja na badala ya Neno. Rudini, enyi watu. Rudini.

204 Angalieni, huko nje kwenye umati uliochanganyikana, sikusema hili. Ni kati yenu, ninyi Wapentekoste mnaoketi hapa, na sisi. Hatuji hapa tupate kusikiwa. Mimi huja hapa kujaribu kusaidia. Naja. Iwapo mimi—iwapo ninasimama tu hapa, kusema ni—nilizungumza juu ya somo fulani asubuhi ya leo, hiyo inanifanya mnafiki. Naja hapa na Ukweli, na ukweli ninaowatakeni mjue, jambo ambalo ninaamini Mungu huliweka moyoni mwangu, kuwasaidia ninyi, ili tuweze kuona saa tunayoishi. Mnaona?

205 Kuna kongamano la Gethsemane, wakati Mtu pekee ambaye angeweza kufa alifikia saa hiyo. Ndipo hapo wakati huo mkuu ulipowadia, hapo ilimlazimu kufanya uamuzi Wake wa mwisho. Hapana shaka Baba alisema, “Je! ungali tayari kupitia jambo hili, Mwanangu?”

206 Akasema, “Hivi inawezekana, Baba, kuna mtu mwingine ambaye Wewe ungeweza kumpata mahali fulani? Ninawapenda watu Wangu. Ninawapenda ndugu wale ambao umenipa Mimi. Inawezekana kwamba mtu mwingine angeweza?”

207 “La. Wewe Ndiwe pekee unayeweza kulifanya. Wewe Ndiwe pekee uliyezaliwa na bikira. Wewe Ndiwe pekee uliyezaliwa pasipo kujuana kimwili.” Hakuna mtu mwingine, hakuna askofu, hakuna papa, hakuna kadinali, hakuna chochote kinachoweza kukusaidia. Ni Huyu. “Wewe Ndiwe pekee unayeweza kulifanya.” Ndipo kongamano likawa.

208 Shetani alikuwa amesimama hapo, tayari kudai jamii ya binadamu. Alisema alikuwa na haki kwa sababu walikuwa wametenda dhambi.

209 Kama vile ninyi watu mliopo hapa, mmezisikiliza zile kanda juu ya ile Mihuri Saba. Wakati Mwana-Kondoo alipojitokeza kudai ukombozi Wake, kile alichokuwa amekomboa, wakati ulimalizikia hapo. Yuko kazini sasa, akifanya kazi ya ukombozi. Lakini siku moja ataondoka kwenye madhabahu, kukitwaa Kitabu cha ukombozi ambacho amekinunua kwa Damu Yake Mwenyewe, ndipo saa imekwisha. Yeye anatokea basi kudai kile ambacho Yeye amekomboa.

210 Alikuwa ndiye Huyu hapa, amesimama Gethsemane, yale mateso makubwa. Dhambi ya kila mtu ilikuwa juu Yake. Kila kitu kilichowahi kufa, mauti ya hicho yaliwekwa juu Yake. Na Yeye alikuwa asiye na hatia, bali ilimlazimu kufanyika dhambi.

211 “Unaweza Wewe, Mwana mtakatifu wa Mungu, kuichukua dhambi ya uzinzi? Unaweza kuichukua hiyo dhambi, adhabu ya

uzinzi? Unaweza kuchukua dhambi, adhabu ya uongo? Unaweza kuchukua dhambi ya mambo haya yote? Pia waweza kuzichukua juu ya nafsi Yako, hata hivyo ukiwa bila hatia?" Alikuwa Ndiye wa pekee. Hilo kongamano lilitimizwa.

Yeye alisema nini? "Si mapenzi Yangu; Yako yafanyike."

²¹² Ee Mungu, je! sisi sote tunaweza kulifikia kongamano la Gethsemane, ule uchunguzi wa mwisho?

²¹³ Ndipo likaja kongamano lingine wakati mmoja. Siku chache baada ya hapo, yapata siku arobaini, likaja kongamano, baada ya kifo Chake, kuzikwa, na kupaa. Kanisa la Kikristo lilikuwa linaenda kufanywa dhehebu.

²¹⁴ Wamethodisti, Wabaptisti, Presbiteri, Lutheri, sisi sote, sikilizeni sasa kwa dakika moja tu, katika kufunga.

²¹⁵ Palitokea wakati ambapo Mungu alikuwa anaenda sio tu kuwachukua watu. . .

²¹⁶ Kama vile, Israeli ni watu Wake. "Israeli itaokolewa kama taifa," Biblia ilisema hivyo, "itazaliwa katika siku moja." Mungu huwashughulikia Israeli kama wa- . . . taifa, kama—kama watu.

²¹⁷ Lakini Yeye hulishughulikia, Kanisa, na mtu binafsi. "Ameita, kutoka kwa Mataifa, watu kwa ajili ya Jina Lake."

²¹⁸ Sasa, tunakuta kwamba saa imewadia sasa. Kanisa hili linapaswa kuendeshwaje? Walikatazwa, ingawa walikuwa wamehubiri, ingawa walikuwa wameponya. . . Nisikilizeni. Ingawa yeye, walikuwa wamehubiri, ingawa walikuwa wameponya, ingawa walikuwa wameona ishara kuu na maajabu, na ingawa walikuwa ni shahidi ya kwamba Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu, hata hivyo aliwakataza kuhubiri mpaka walipofanya kongamano hili. "Ngojeni pale juu kwenye mji wa Yerusalemu. Nitawatumia neno jinsi kanisa la Kikristo linavyopaswa kuendeshwa. Nitawajulisha kama itanibidi kuwa na askofu, ama kadinali, ama papa, ama chochote nitakachokuwa nacho. Nitawatumia. Ninaenda Mbinguni, kufanya kongamano. Mtangojea huko mpaka mtakaposisia matokeo." Amina. Amina.

²¹⁹ Ninakumbuka wakati walipokuwa wakifanya lile kongamano la Geneva, maskini rafiki yangu mhudumu, Dk. Pettigrew, huko Louisville, alisema alikuwa akisikiliza radio, akiisikiliza. Taifa lilikuwa hatarini. Alitaka kuona kile uamuzi ulikuwa, kile walichokuwa wanaenda kufanya. Ndipo kijana mamboleo akaja mlangoni, huku nywele zake zinaning'inia usoni mwake, na kusema, "Dk. Pettigrew, ninasikia ya kwamba wewe ni. . . kwamba ni mtu mwenye ushawishi." Kasema, "Mimi, nina nyimbo fulani za roki. Wa—watu hawatanisikia. Laiti ungenipiga tu jeki kidogo!"

²²⁰ Akasema, “Mwanangu, simama hapo nje kidogo tu.” Kasema, “Nina—ninasikiliza nione yale matokeo yatakayokuwa.”

²²¹ Akasema, “Lakini, Dk. Pettigrew,” kasema, “hili ni jambo kuu.” Akasema, “Hili linamaanisha mengi sana kwangu mimi.” Kana kwamba lilimaanisha mengi kuliko kusikiliza matokeo kutoka kwenye lile Kongamano la Mabingwa Wanne?

²²² Hivyo ndivyo watu walivyo leo hii. Maskini kijana mamboleo, kitu kingine, katika jina la—la dini wanakuja huku na kujaribu kuvutia usikivu wenu kutoka kwa yale Matokeo halisi. Hum! Maskini dondoadume, waliodhalilishwa, wakafanywa wa kidini (iwapo kuna neno kama hilo la kutumia), kupata wafuasi wengi zaidi na watu bora zaidi, kupata kanisa kubwa zaidi na wafuasi wengi zaidi, wakijaribu kuuvutia usikivu wenu, ndugu. Msiwasikilize. Tunayo Matokeo yameandikwa *Hapa*.

²²³ Hilo lilikuwa ni kongamano la pentekoste. Kasema, “Msiimbe wimbo mwingine, msihubiri neno jingine, bali pandeni mwende kule mkangoje mpaka kongamano hili litakapokwisha. Nitawatumia Habari hizo. Nitawaambia ni nani aliye mkuu kuliko wote miongoni mwenu. Nitawaambieni yale hasa mnyapaswa kufanya; kama mtakuwa na dhehebu, kama mtakuwa na papa, ama askofu, ama chochote mnachopaswa kuwa nacho. Nitawaambieni habari zake. Lakini ngojeni mpaka mtakaposikia Matokeo. Tunaenda Mbinguni, kuamua jambo hili.”

²²⁴ “Naye akapaa Juu, akateka mateka, akaketi kwenye mkono wa kuume wa Mungu, kisha akawatumia wanadamu vipawa.” Ndipo wakati Siku ya Pentekoste ilipotimia kikamilifu, wao walikuwa wakingoja.

²²⁵ Loo, vipi kama ingalikuwa, vipi kama—kama Andrea angalisema, baada ya yapata siku sita, “Mwajua, ndugu, ninaamini haitubidi kungoja muda mwingi zaidi. Ninaamini ya kwamba, kwa imani, tunapokea huduma yetu. Tunapaswa kuendelea, tuanze mara moja na kuanzisha huduma yetu, sasa hivi.”

²²⁶ Hiyo ndiyo shida ya wahudumu wengi. Hakai pale muda mrefu kutosha, mpaka ayasikie Matokeo, mpaka alisikie agizo lake.

²²⁷ Vema, mwajua, labda kungekuwako na jina jingine, Filipino, angeamka, kasema, “Mnajua, nimekuwa nikijisikia vizuri sana. Hata hivyo, tuna maarifa ya jambo hili, kile Yeye anachotaka kufanya.”

²²⁸ Hilo huenda ikawa hivyo, ndugu zangu. Huenda ukawa na B.A., D.D., L.L., Q.U.S.T., na hiyo haitamaanisha kitu. Maarifa yako hayamaanishi kitu. Seminari zako zote hazimaanishi kitu. Inakupasa kungoja Matokeo, kuona kile alichosema Mungu. Na

hakuna mtu aliye na haki ya kuhubiri Injili pasipo kukutana, kwanza kukutana na Yesu Kristo kama Mtu, sio kama theolojia fulani, theolojia. Vema, mnajua ninachomaanisha, digrii fulani ya theolojia. Digrii ya theolojia, hana haki yoyote kufanya hivyo juu ya hiyo, haijalishi jinsi anavyoweza kulielezea Hilo. Hilo silo.

²²⁹ Kama tu vile Musa. Yeye angaliweza kuwafundisha Wamisri hekima. Alikuwa ndiye mtu mwerevu kuliko wote nchini, bali ilimbidi kuingia katika kongamano na Mungu. Na hakuna mwanaume aliye na haki ya kudai kuwa Mkristo, hakuna mwanamke, hakuna mtoto, hakuna mhubiri, hasa, mpaka yeye mwenyewe amekuja kwenye mchanga huo mtakatifu ambapo alikutana na Mungu. Wanatheolojia wote ulimwenguni, makafiri wote ulimwenguni, hawawezi kulielezea hilo vibaya kwake. Yeye alikuwa hapo. Lilitukia. Lilimfanyikia yeye. Yeye anajua mahali anaposimama.

Hapo, walienda kwenye Siku ya Pentekoste.

²³⁰ Nasi hatukuona ninii—ninii... Sasa, mimi si... Ninatoa tu tamshi. Hatulioni pale, ambapo askofu alijitokeza barabarani akiwa na mkoba wake mkononi mwake, naye akasema, “Sasa, nimetumwa na Bwana. Ninataka kuwawekea mikono enyi ndugu na kuwatumia nje.” Hilo ndilo toleo lake la 1963, askofu na fimbo yake.

²³¹ Vema, tunawazia habari zao. Hebu tulichukue tu pamoja na heshima inayowastahili marafiki zetu Wakatoliki. Hebu tuseme kasisi alipanda kuja barabarani, akiwa na desturi za ibada ya mwisho, zinavyoitwa. “Toa ulimi wako na ule mkate mwembamba, nami nitakunywa divai. Ndipo utakuwa mfuasi.” Kama hilo lingewezekana, lingekuwa kule kwanza.

²³² Mungu hana kikomo. Uamuzi Wake ni kama tu ulivyokuwa katika bustani ya Edeni. Yeye, uamuzi Wake wa kwanza, unatosha.

²³³ Vema, walifanya nini? Walingojea, na wakangojea, na hawakuridhika. Walingojea, mpaka, “Kukaja sauti kutoka Mbinguni kama upepo mkuu ukienda kasi. Ukaijaza nyumba yote walimokuwa wameketi. Ndimi zilizogawanyika zikawakalia juu yao, kama Moto. Na wote wakajazwa na Roho Mtakatifu, na wakaanza kunena kwa lugha zingine, kama Roho alivyowajalia kunena.”

²³⁴ Kundi la waoga walioogopa uinjilisti, kundi la waoga walioogopa kukabiliana na watu wenye vyeo na wenye sifa wa mji na wakosoaji wa kidini, walikuwa huko nje mtaani, wakishuhudia, “Hili ni Lile.” Huo ulikuwa ni uamuzi wa Mungu.

²³⁵ Siku chache baada ya hapo, Wasamaria. Filipo alikuwa ameenda huko chini na kuwahubiria na kuwabatiza katika Jina la Yesu Kristo, ingawa Roho Mtakatifu hakuwa amemshukia yeyote wao bado. Kwa hiyo, wakatuma habari kwa Petro na kumleta huko. Walijua walikuwa na furaha kuu. Walikuwa na

furaha na kushangilia, nao walikuwa na wakati mzuri sana. Na walishakuwa na uponyaji mkuu na kila kitu.

²³⁶ Sasa, ndugu wa Nazarayo, Pilgrim Holiness, Methodisti, sikilizeni. Uponyaji sio. Furaha siyo. Ni ule ujuzi. Ni Roho Mtakatifu, Kristo Mwenyewe, akiingia ndani yako, kama Mtu.

²³⁷ Waliagizia na kumleta Petro na Yohana walioshuka wakaja na kuweka mikono yao juu yao, ndipo Roho Mtakatifu akaja juu yao. Katika Matendo 10:49 tunaona kwamba Petro, wakati alipokuwa akizungumza na Wamataifa, “Wakati Petro akali akisema Maneno haya, Roho Mtakatifu akawashukia hao waliolisikia Hilo. Kwa kuwa waliwasikia wakisema kwa lugha, na kumtukuza Mungu. Ndipo Petro akasema, “Tunaweza kuzuia maji, kwa kuwa hawa wame—wamempokea Roho Mtakatifu kama sisi tulivyompokea hapo Mwanzo?”

²³⁸ Paulo, akizungumza na kundi la Wabaptisti, katika Matendo 19, alipitia kwenye pwani ya juu ya Efeso. Anakutana na baadhi ya wanafunzi. Walikuwa na furaha. Walikuwa na mhubiri mkuu wa Kibaptisti pale, jina lake Apolo. Naye alikuwa mwanasheria aliyeongoka. Ndipo akasema, “Alikuwa akithibitisha kwa Biblia, ya kwamba Yesu alikuwa ndiye Kristo.”

²³⁹ Ndipo Akila na Prisika, watentengezaji wa hema pamoja na Paulo, kasema, “Ndugu yetu Paulo yuko gerezani kule chini.” Si hapo ni mahali pa mhubiri kuwa? Alikuwa gerezani kwa sababu alitoa pepo kutoka kwa mpiga ramli. Naye akasema, “Yeye, yuko gerezani, bali atatutembelea karibuni sana, naye atawaelezeeni Neno la Mungu, kikamilifu zaidi.”

²⁴⁰ Nao walikuwa na wakati mzuri, kama vile Wabaptisti wote wazuri wanavyokuwa nao, kupiga makelele, kumsifu Mungu, wakiwa na uponyaji, na ishara, na kadhalika.

²⁴¹ Lakini Paulo alipokuja na kuwasikiliza, mtume, yeye alisema, “Mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?” Walidhani walikuwa Naye. Mnaona? “Tangu mlipoamini?” Tunafikiri, tunapoamini tumempokea Huyo. Hilo ni kosa. Alisema, “Mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?”

Wao wakasema, “Hatujui ni kitu gani, ama kama kuna Mmoja.”

Akasema, “Mlibatizwa kwa ubatizo gani?”

Kasema, “Wa Yohana.”

Akasema, “Huo hautafanya kazi tena. Mnapaswa kubatizwa tena.”

²⁴² Kwa hiyo, akawabatiza katika Jina la Yesu Kristo. Akaweka mikono yake juu yao, ndipo Roho Mtakatifu akaja juu yao, nao wakanena kwa lugha na kumtukuza Mungu. Vipi? Kama tu walivyofanya hapo mwanzo. Fomula ile ile ilitekelezwa.

²⁴³ Daktari anapoandika maagizo, usiache mmoja wa hawa wauza madawa matapeli ayachezee. Watakupa kiuasumu kingi kupita kiasi, hakitakusaidia. Na kama wakiweka sumu nyingi kupita kiasi, itakuua.

²⁴⁴ Usiichezee fomula ya Mungu. Itekeleze jinsi ilivyokuwa katika lile kongamano. Hayo yalikuwa ndiyo Maagizo. Amina. Ninampenda.

²⁴⁵ Inanikumbusha juu ya wazazi wa Yesu. Walipanda wakaenda kwenye karamu ya pentekoste. Walipokuwa njiani wakirudi waligundua. Walishakuwa siku tatu au nne, na hawakumpata Yeye miongoni mwao. Wakaanza kushangaa.

²⁴⁶ Hivyo karibu ndivyo ilivyo sasa. Makanisa yanaanza kugundua, “Nini kilimpata Yesu? Ni nini kilifanyika? Sisi ni Wapentekoste, lakini kulifanyika nini? Sisi ni Wamethodisti, lakini kulifanyika nini? Nini kilimpata Yesu?”

Wakaanza kutafuta miongoni mwa jamaa zao.

²⁴⁷ Hivyo ndivyo tunavyoanza kufikiria. “Moody alisema nini? Sankey alisema nini? Finney alisema nini?” Hiyo ilikuwa ni siku yao. Tumepiga hatua mbele. Kama tukianza kutafuta huko nyuma, kama wao walivyofanya!

²⁴⁸ Walienda kwa jamaa zao na wasingeweza kumpata. Walienda kwa jamaa zao wote, maaskofu, na kadhalika. Wasingeweza kumpata. Hatimaye, wakampata pale pale tu walipomwacha. Walimwacha wapi? Kwenye karamu ya pentekoste. Iliwabidi kurudi njia yote mpaka mahali walipomwacha, kabla hawajampata.

²⁴⁹ Basi, kanisa, hivyo ndivyo inavyotupasa kufanya, kurudi mahali tulipomwacha. Tuyaondokee baadhi ya mapokeo yetu. Turudi mahali tulipomwacha. Mnataka kujua mahali mlipomwacha? Fanyeni kongamano dogo la Biblia na msikate tu kona yoyote, semeni tu Kweli.

²⁵⁰ Tutangojea sasa mpaka tutakapoona jinsi ilivyokuwa. Hakuna maaskofu, hakuna chochote, Roho Mtakatifu tu ndiye aliyepaswa kuliongoza Kanisa. Huyu ndiye Kiongozi pekee tuliye naye ni Roho Mtakatifu, na Yeye huongoza kulingana na Neno.

²⁵¹ Kama ukisema, “Vema, ninaye Roho Mtakatifu,” nawe unalikana Neno; si Roho Mtakatifu basi, maana Roho Mtakatifu aliiandika Biblia. Kweli. Kwa hiyo, si Roho Mtakatifu.

²⁵² Sikilizeni. Ninafunga. Katika makongamano ya ulimwengu, wao hufanya nini? Wanakula pamoja. Wanazungumza pamoja. Wanabishana. Wanadanganyana, kwenye kongamano la ulimwengu, kongamano la ulimwengu, la mataifa.

²⁵³ Lakini nini, wakati Mungu anapoitisha kongamano, kumefanyika nini? Wanakutanika pamoja. Hawafanyi karamu,

bali wanafunga. Hawagombani, bali wanaomba. Wanangojea mpaka wapate maagizo, ndipo wanasonga mbele.

²⁵⁴ Hilo ndilo kanisa linahitaji leo hii, ni kusonga mbele, kupata Maagizo. Nawe unasema, “Ninawezaje kupata Maagizo?” *Haya* hapa. *Hii* ndiyo hayo Maagizo. “Unajuaaje, Ndugu Branham?” Jinsi Mungu alivyopanga ukombozi kwanza ilikuwa ni kwa damu, na Yeye kamwe hataibadilisha, wakati Mungu anapofanya uamuzi. Hiyo ndiyo sababu unaweza kuning’iniza nafsi yako kwenye hiyo Biblia, fungu lolote la maneno Hiyo isemayo, kwa sababu Hiyo ni Neno la Mungu.

²⁵⁵ Naye Mungu, akiwa hana kikomo, Yeye hawezi kusema, “Vema, nilikosea, miaka elfu mbili iliyopita.” Mungu ni wa Milele. Kamwe hakuanza. Kamwe hatakuwa na mwisho.

²⁵⁶ Na njia pekee unayoweza kuwa kama Yeye ni kuwa sehemu Yake. Kwenye Siku ya Pentekoste . . .

²⁵⁷ Ile Nguzo kuu ya Moto iliyokuwa imewafuata Israeli, ama Israeli walikuwa wameifuata kupitia nyikani, mnaona, ile Nguzo kuu ya Moto ilikuwa ni Mungu, Malaika wa agano, Yesu Kristo. Musa alihesabu shutuma la Kristo kuwa ni hazina kuu kuliko ile ya Misri, kwa hiyo akaiacha Misri na kumfuata Kristo.”

²⁵⁸ Angalieni, kwenye Siku ya Pentekoste, Mungu alifanya nini? Yeye aliichukua ile Nguzo kubwa ya Moto na kuigawanya. Hiyo ilikuwa ni Yeye Mwenyewe. Ndimi za Moto, ndimi zilizogawanyika, ndimi zilizogawanyika, zilishuka, ndimi zilizogawanyika, na kukaa juu ya kila mmoja.

²⁵⁹ Loo, hivi haitupasi kujionea aibu, kuyaacha madhehebu yetu yatugawanye! Wakati, Mungu alijigawa Mwenyewe miongoni mwetu, ili tuweze kuwa mmoja. “Hivi watu wote watajua ya kwamba nyinyi ni wanafunzi Wangu.” Mnasikia hilo, ndugu na dada? Mungu alijigawa Mwenyewe. Sisi kamwe hatutenganishwi, mmoja na mwingine, kwa kuwa sisi ni sehemu za Mungu.

²⁶⁰ Hebu Moto huu uje tu kwenye Moto huu, na, baada ya kitambo kidogo, mtaona, utausogeza huo. Umekuja kupitia Luther, Wesley, Pentekoste. Basi mtaona, ile piramidi itafunikwa, moja ya siku hizi.

²⁶¹ Mnajua, kamwe haikufunikwa, ile piramidi nyuma ya dola yako. “Ule muhuri mkuu,” inasema. Na sisi katika Marekani, huu hapa muhuri wa Marekani upande *huu*. Lakini kwa nini ikasema, “Ule muhuri mkuu,” ule ambao Henoko alitengeneza? Sio mafundisho ya piramidi sasa, maana siamini katika upuuzi wa namna hiyo. Lakini wao kamwe hawakuifunika piramidi. Kwa nini? Ji—Jiwe la kifuniko lilikataliwa. Lakini Hilo litakuja tena, siku moja. Bwana asifiwe!

²⁶² Na, unaona, katika piramidi hiyo, nimekuwa kule. Imechongwa vizuri sana hata huwezi kuingiza wembe. Hakuna

saruji kati yake. Inakaa pamoja kikamilifu tu kama kwamba ni jiwe moja.

263 Basi wakati Kanisa hilo litakapochongwa likawa sura kamilifu ya Yesu Kristo, Yeye atakuja, awafufue watakatifu wote hapo Yeye atakapokuja, na kuwachukua pamoja na Yeye. Kanisa la Mungu aliye hai litanyakuliwa.

264 Lakini, ndugu zangu, hatutakuwa kama Hawa, mmoja kuwa na *hili* na mwingine kuwa na *lile*, mwili uliounduka. Itakuwa ni neno kwa neno, yale Mungu aliyosema.

265 Mwasema, “Ndugu Branham, Yeye alisema nini basi? Wewe kamwe hukutwambia.”

266 Vema. Petro alilineni. Walipotaka kujua, “Tunaingiaje katika hili? Kulifanyika nini?” Yeye alitupatia fomula.

267 Sasa, kama alisema, “Peana mikono na ujiunge na kanisa,” hivyo ndivyo ingekuwa. Na kama alisema, “Simama kwa kichwa chako,” hivyo ndivyo ingekuwa. Alisema, “Tutamwandaa mtu mashuhuri, na kufanya shirika kubwa, na papa mkuu, na *hili*, *lile*, kubwa,” hivyo ndivyo ingalikuwa.

268 Lakini alisema nini? “Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa wote walio mbali, hata wote watakaotwa na Bwana Mungu wetu wamjie.”

269 Na mradi tu Mungu anaita, haina budi kuwa ni fomula ile ile. Sio kupeana mikono, kurudia kanuni ya imani; bali kubatizwa na Roho Mtakatifu, katika Mwili wa Yesu Kristo. Hivyo ndivyo Kanisa la Kikristo lilivyopaswa kuendeshwa. Sio kwa kanuni za imani, sio kwa dhehebu, sio kwa elimu, sio kwa theolojia; bali kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, kuwaongoza wanaume na wanawake. Na Yeye kamwe hatakuongoza akuondoe kwenye Neno la Mungu. Yeye atakuongoza moja kwa moja kwenye Neno la Mungu, kwa sababu “Mtu hataishi kwa mkate pekee, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu.”

270 Hivi mna yapata dakika mbili ama tatu zaidi, nne? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Nina kongamano lingine ningetaka kuwakumbusha. Nimeliandika hapa. Ni ninii tu, “Matendo 4,” inasema. Ninajua kile hilo linachomaanisha.

271 Matendo 4, baada ya wanafunzi kuanza kuhubiri, makanisa yalianza kukosoa. Walianza kuwafanya... Hayo makanisa yalisema, “Sasa ngojeni kidogo. Mnaweza kuendelea na kufanya miujiza yenu. Mnaweza kufanya jambo hili lote, bali kamwe msihubiri tena katika Jina la Yesu Kristo.” Wakawapiga, na kwa mijeledi, na kila kitu kingine. Kwa hiyo walifanya nini? Jambo fulani halina budi kufanywa. Wamekatazwa. Sheria inasema hawawezi kuhubiri jinsi hii tena.

272 Loo, ndugu! Laiti ningalikuwa tu na muda zaidi kidogo. Wakati unakuja ambapo ama utaliweka dhehebu lako katika Baraza la Makanisa Ulimwenguni, utaninii... Kama ukifanya hivyo, unachukua sanamu ya mnyama, maana mna mamlaka kama tu ilivyokuwa katika Rumi. Na kama hutafanya hivyo, utakuwa mtu binafsi, kanisa linalosimama peke yake; na ukifanya hivyo, ile sanamu ya mnyama itafunga milango yako, nawe utakatazwa. Ndipo utahitaji kongamano. Unaona?

273 “Wanatwambia ya kwamba hatuwezi, hatuwezi tena. Hatuwezi kuhubiri katika Jina la Yesu. Hebu na tumtake shauri Mungu na tupate kujua kama tunaweza, ama hatuwezi.” Kwa hiyo walipanda wakaenda na kufanya kongamano. Loo, loo, loo, loo! Samahani. Tunahitaji moja kama hilo, asubuhi ya leo. “Ni vema kwetu kumtii mwanadamu, ama Mungu?” kasema yule mtume. Walikuwa na kongamano, karibu kama lile tulilo nalo asubuhi ya leo. Nao wakasimama na kutoa, “Ka—ka—kanisa linatwambia hatuwezi kuhubiri isipokuwa tuje katika kundi lao, na kadhalika. Na hatuwezi kuwa na mhudumu *huyu* ’sipokuwa dhehebu liseme hivyo. Na haijalishi limetiwa mafuta kiasi gani, inatubidi kufanya *hili, lile*.” Nanyi mnajua jinsi ilivyo, kila kundi, na kadhalika. “Tutafanya nini?”

274 Basi walifanya kongamano, na wakapiga magoti na kuanza kuomba. Hilo ni kongamano la Matendo 4. “Basi walipofanya hivyo, wote kwa moyo mmoja, ‘Bwana, kwa nini watu wakawaza ubatili; ama mataifa yakaghadhabika, nao watu wakawaza ubatili? Nyosha mkono wa Mtoto Wako Mtakatifu Yesu, kuwaponya wagonjwa. Tumekatazwa kufanya jambo hili.’ Nao wote wakiomba kwa moyo mmoja.”

275 Mnazungumza, watu wengine, wanatukosoa kwa ajili ya kila mtu kuomba wakati ule ule. Ungeonaje kuwa katika kundi hilo, “Wote kwa moyo mmoja?” Mtu fulani alisema, “Mungu anawezaje kusikia hayo?” Unafikiri Yeye anayasikia maombi mangapi kwa wakati mmoja, hata hivyo? Unasahau. Yeye si mwenye kikomo. Yeye hana kikomo. Unaona?

276 “Basi wote walipoomba kwa moyo mmoja,” Biblia ilisema, “lile jengo lilitikisika ambamo walikuwa wameketi pamoja.” Amina. Yale Matokeo yakarudi. “Nao wakaondoka wakaenda wakimhubiri Yesu Kristo, kila mahali, Mungu akitenda kazi pamoja nao, akilithibitisha Neno.” Kongamano la Matendo 4.

277 Loo, ndugu, hebu kidogo, kuna kongamano lingine. Huenda hukuhudhuria lolote la makongamano haya. Huenda hukuhudhuria makongamano haya ya ulimwenguni. Kumbuka, huenda hukuyahudhuria. Lakini, kumbuka, kuna kongamano moja, ninaloenda kulizungumzia sasa, ambalo utahudhuria. Sijali wewe ni nani, utalihudhuria. Huenda ukawa na udhuru, mpaka wakati huu, lakini tangu sasa na kuendelea huna udhuru. Hilo ni lile kongamano kwenye Hukumu. Hiyo ni kweli.

Nyote mtakuwako, kila mmoja wetu. Na tutatoa hesabu ya yale tumefanya na kusema humu duniani. Hilo ni kongamano moja utakalohudhuria.

²⁷⁸ Kila wakati unaposikia king'ora kikiteremka barabarani, kumbuka, kinakutia alama. Hutakuwa hapa muda mrefu sana. Ambapo unaona unywele wenye mvi ukitokea, kuinama kwa mabega, ukiona hospitali, makaburini, ni kitu gani? Ushuhuda, huko hapa kwa wakati wote, nawe unasongea kwenye hilo kongamano. Na sote tutakuwa huko.

²⁷⁹ Itatubidi kutoa hesabu kwa yale tumefanya na Yesu Kristo. Hiyo ni kweli? Naye Yesu Kristo ni Nani? Neno. "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwako pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili akakaa miongoni mwetu." "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele."

²⁸⁰ Mungu, akitenda kazi katika vipindi vitatu vya wakati, hiyo ndiyo sababu Yeye alinena kuhusu kumwita Yeye "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu." Mnaona? Sio Miungu watatu mbalimbali. Hapo ndipo mnapochanganyikiwa. Sio Miungu watatu mbalimbali. Ni Mungu mmoja katika madhihirisho matatu, mnaona, ya—ya Mungu huyo mmoja. Tuna Mungu mmoja tu. Sisi si makafiri. Mnaona? Lakini tu—tuna Mungu mmoja, bali madhihirisho matatu. Hiyo ndiyo sababu Mathayo alisema, "Mwabatize katika Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," kwa sababu, mnaona, Hilo lilikuwa ni Moja. Mungu yule yule: aliyekuwa katika Agano la Kale; ndiye Mungu yule yule aliyedhihirishwa; na ndiye Mungu yule yule aliye hapa leo hii. Yesu Kristo, yeye yule: ambaye Musa aliuacha u—ulimwengu huko Misri; yuyo huyo basi alikuwa hapa leo hii; na yuyo Huyo atakuwako milele, Yesu Kristo. Na Yeye ni Neno. Amina.

²⁸¹ Mungu hana budi kulihukumu kanisa kwa kitu fulani. Mungu hana budi kuuhukumu ulimwengu kwa kigezo fulani. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema, kama atauhukumu kwa kanisa, ni kanisa lipi? Kama akiuhukumu kwa la Katoliki ya Kirumi, la Kiyunani limepotea. Kama akiuhukumu kwa la Kiyunani, la Kirumi limepotea. Kama akiuhukumu kwa la Kimethodisti, la Kibaptisti limepotea. Kama akiuhukumu kwa la Kibaptisti, la Kimethodisti limekwisha; vinginevyo. Kama akiuhukumu kwa la Umoja, la Uwili limekwisha. Kama akiuhukumu kwa Uwili, la Utatu limekwisha. Kama akiuhukumu kwa la Utatu, yote mawili yamekwisha. Haya basi. Ni kitu gani? Ni kitu gani, ndugu zangu? Ni lundo la upuuzi.

²⁸² Mungu hana budi kuwa na kigezo fulani. Kama ilinibidi kujiunga na kanisa, ningejiunga na lipi? Kunalo Moja tu, na hujiungi na Hilo.

283 Nimekuwa katika familia ya Branham, miaka hamsini na minne, na kamwe sikuwahi kujiunga na familia hiyo. Nilizaliwa wa Branham. Mimi ni wa Branham kwa maana baba yangu ni Branham.

284 Na mimi ni Mkristo kwa sababu Baba yangu ni—ni Mungu. Amina. Sisi ni Wakristo juu ya msingi huo. Sisi ni Wakristo. Tumezaliwa kwa Roho Wake. Nayo Roho ya Baba yangu, ndani yangu, ninazo sifa za Mungu ndani yangu, nazo zinajionyesha zenyewe kama zilivyofanya katika Mwana Wake, Yesu Kristo. Haya basi.

285 “Juu ya mwamba huu ninalijenga Kanisa Langu. Sio kwa . . . Mwili na damu havijakufunulia hili, bali Baba Yangu aliye Mbinguni amelifunua. Juu ya mwamba huu ninalijenga Kanisa Langu.”

286 Kama Mungu akiuhukumu ulimwengu kwa kanisa Katoliki, la Protestanti limepotea. Akiliunganisha na—na la Waprotestanti, lipi? Akihukumu kwa kanisa Katoliki, kuna hofu nyingi mbalimbali za milki za kanisa Katoliki, kwa hiyo itakuwa ni lipi? Mnaona, mtu angechanganyikiwa. Usingeweza kujua la kufanya.

287 Lakini hili hapa kile Mungu atawahukumu kwalo, Neno. Hicho ndicho kigezo. “Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitashindwa kamwe.” Juu ya Hili ninachukua msimamo wangu. Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao. Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao.

Juu ya Kristo, Mwamba wenye imara,
nasimama;

Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao.

288 Ninalitegemea Hilo. Situmainii kile nilicho mimi. Ninatumainia kile Yeye alichoko. Siwezi, siwezi kwenda Mbinguni; Yesu alisema ilibidi niwe mkamilifu kwenda Kule. “Iweni basi wakamilifu kama Baba yenu aliye Mbinguni alivyo.” Unawezaje kuwa? Lakini unapokuwa . . . Usijiangalie wewe, bali Dhabihu yako.

289 Vema, kama nyumbu mdogo alizaliwa wakati wa Agano la Kale. Alikuwa na masikio yaliyovunjika yakainama, na magobwe, na mkengeza. Mbona, alijua atapigwa kichwani. Hafai kitu. Ila mama angeweza kumwambia, “Mwanangu, ulizaliwa ukiwa na haki ya mzaliwa wa kwanza. Kwa sababu kuwa ulizaliwa hivyo, hivi, utaishi. Lakini yule atakayekufa kwa ajili yako itambidi kuwa ni mwana-kondoo mkamilifu, itabidi atolewe kusudi upate kuishi.” Wataivunja shingo ya—ya—ya farasi kama yeye hakuwa mzuri, naye si mzuri. Lakini, unaona, lakini mwana-kondoo mkamilifu hana budi kufa ili yeye aweze kuishi.

290 Kama ukisema wewe hufai kitu, “Sistahili kuponywa, Ndugu Branham. Sistahili kumjia Kristo.” Usijiangalie

mwenyewe. Angalia Dhabihu yako. Mimi sifai kitu. Hakuna kitu kizuri ndani yangu, si hata wazo. Hakuna kitu ambacho si kizuri, hakuna kitu ambacho si kizuri ndani yako. Hakuna yeyote wetu anayestahili chochote ila kuzimu. Hiyo ni kweli.

²⁹¹ Lakini, loo, angalia kile kinachosimama kutuwakilisha sisi. Angalia kile kinachosimama kutuwakilisha sisi. Na *Hapa* ni Maisha Yake, katika maandishi, yanayojaribu kudhihirishwa kupitia sisi. Halafu basi, kupitia maskini kanuni fulani ya imani, tunalikataa Hilo. Loo, tunahitaji kongamano. Naam.

²⁹² Hiyo ndiyo sababu ninaweza kwenda jukwaani, pasipo na woga kwamba jambo fulani litainuka, na litafanyika *hivi*, ama *vile*, ama litashindwa, ama jambo fulani litaenda kombo. La. Ninaiangalia Dhabihu yangu.

“Billy, ulifanya nini juma hili?”

²⁹³ Nilifanya ya kutosha kufa, kasema, katika saa moja. Mimi, mimi ni mwenye dhambi, kwa kuanzia. Lakini ninamwangalia Yule aliyenipa ahadi. Ninamwangalia Yule aliyesema hivyo, “Usiogope. Simama pale. Kwa kusudi hili ulizaliwa. Nilikuinua kwa kusudi hili.” Basi pepo wote kuzimuni hawawezi kunisogeza. Ninasimama pale juu ya Kristo, ule Mwamba wenye imara.

²⁹⁴ Hivi yeyote wenu anamkumbuka Paul Rader? Shujaa mashuhuri wa Mungu. Nilikuwa mvulana mdogo, nikiketi miguuni pake. Alikufa, hapa California, si muda mrefu uliopita. Wakati alipokuwa akifa. . . Yeye na ndugu yake Luke walishikana pamoja, kama mimi na mwanangu hapa. Walienda pamoja, pamoja tu, kama ndugu na ndugu, kama tu baba na mwanawe. Ndipo Paul akafikia mwisho wa safari yake.

²⁹⁵ Chuo cha Biblia cha Moody kikatuma maskini kundi la waimbaji wanne kule chini, wakaimbe. Nao walikuwa wamevuta mapazia yote, na vikingo vimevutwa, hospitalini. Naye Luke alikuwa na namna fulani ya . . . ninamaanisha, Paul alikuwa na ucheshi, mwajua. Ndipo akaangalia kote kwenye hilo kundi la wanne. Nao walikuwa wakiimba *Karibu Zaidi Na Wewe Mungu Wangu*. Akasema, “Nani anayekufa, mimi ama nyinyi?” Akasema, “Yafungueni hayo mapazia hapo na mniimbie baadhi ya nyimbo nzuri, changamfu za Injili.” Ndipo wakaanza kuimba:

Msalabani alipofia Mwokozi wangu,
Kule chini nilipolia nisafishwe kutokana na
dhambi;

Hapo moyoni mwangu kulitiwa Damu;
Utukufu kwa Jina Lake!

²⁹⁶ Akasema, “Huo wasikika bora zaidi.” Kasema, “Yuko wapi Luke, yule aliyeshikamana nami kwa heri na shari.”

²⁹⁷ Asingeweza kumwona ndugu yake akifa. Alikuwa kwenye chumba hicho kingine. Wakaenda wakamleta. Paul akamwinulia

Luke mkono wake mkubwa, naye Luke akaushika mkono wake. Machozi yakatiririka shavuni mwake.

²⁹⁸ Kasema, “Luke, hebu liwazie. Tumekuwa pamoja muda mrefu sana. Tumepitia mafungu mengi ya miiba, na kupitia mashimo mengi. Lakini, hebu liwazie, katika dakika tano kuanzia sasa nitakuwa nimesimama katika Uwepo wa Yesu Kristo, nimevikwa haki Yake.” Jambo ndilo hilo.

²⁹⁹ Paul ameniambia. Kasema yeye . . . wakati alipokuwa kijana mwanamume. Alitoka Oregon. Alikuwa ni bwa—bwana miti, naye angeikata miti. Naye akasema, wakati alipokuwa kwenye moja ya vile visiwa . . . Ninasahau ilikuwa ni wapi. Marekani ya Kusini, huko ndiko ilipokuwa. Naye alikuwa akifanya umishenari kule. Ndipo akashikwa na hii homa mbaya, homa ya maji meusi. Na, loo, mnajua hiyo ni nini. Hiyo ni mauti, mara moja. Huko mbali sana nyikani, maili kadhaa kumfikia daktari.

³⁰⁰ Paul alikuwa mwaminio hodari katika uponyaji wa Kiungu, kama mnavyojua. Na kwa hiyo basi a—akamwambia mke wake, akasema . . . Walikuwa wakienda kumleta daktari. Akasema, “Haitaleti tofauti yoyote. Nisingeweza kuishi muda mrefu hivyo.” Kwa hiyo mke wake . . . Kasema, “Mpenzi, wewe piga magoti hapa chini, kando ya kitanda, ukazungumze na Daktari wetu. Hebu na tumwite Yeye jukwaani.”

³⁰¹ Kwa hiyo mke wake akaanza kuomba, “Mungu, usimwache mume wangu mpendwa afe. Yeye yuko hapa kwenye huduma ya umishenari kwa ajili Yako. Usimwache afe.”

³⁰² Homa ikipanda sana, karibu, amerukwa na akili zake, anaenda tu na kurudi. Akasema, “Mpenzi, kunaingia giza zaidi na zaidi. Siwezi kuishi ila kwa kitambo kidogo tu.” Kasema, “Endelea tu kuomba, mpenzi.”

³⁰³ Ndipo akazimia. Alisema aliota ndoto. Kasema aliota kuwa alikuwa amerudi Oregon, kijana mwanamume. Na akasema alikuwa na bosi kwenye kambi ya wakata miti. Akasema, “Paul, panda juu, juu ya kile kilima pale, ukanikatie mti wa ukubwa fulani uniletee.”

Kasema, “Sawa, bosi.”

³⁰⁴ Basi akapanda juu ya kile kilima, na akasema angeweza tu kuona lile shoka. Mnajua, kadiri unavyozidi kwenda kaskazini, mbona, ndivyo mbao zinavyozidi kuwa nyororo; unavyozidi kwenda kusini, ni ngumu zaidi, mti ule ule. Kwa hiyo, akapanda kule juu. Naye akasema alianza kuona shoka likiingia ndani sana, ncha yake, ndani ya mti, wakati akiukata mti huo. Akaliharibu, na kulitengeneza. Akalichomeka shoka shinani, chini kwenye shina la huo mti, sehemu iliyo kubwa; nayo ilikuwa, mwajua, kuinua, kuweka magoti yake pamoja, kuinua. Kasema yeye ni mtu mwenye nguvu. Mnajua jinsi Paul alivyokuwa, mtu mfupi, mwenye nguvu.

305 Kwa hiyo akaanza kuinua huo mti, na kabisa asingeweza kuuinua. Akasema, “Nilipambana vikali na kujaribu. Na nikajisikia ninii sana. . . Ilinibidi kulipeleka gogo hilo kule chini kwa bosi.” Akasema, “Nisingeweza kabisa kuuinua.” Kasema, “Nikasukuma kwa nguvu, kusukuma kwa nguvu sana na kuvuta, na kusukuma kwa nguvu na kuvuta,” akasema, “mpaka nguvu zangu zote zikaisha kabisa.” Kisha kasema, “Niliketi tu chini nikiegemea mti huo, na kuwaza, ‘Nimechoka sana! Siwezi hata kusogea tena.’”

306 Kasema, “Moja kwa moja nikasikia sauti iliyo tamu kuliko zote niliyowahi kusikia. Ilikuwa ni bosi wangu. Naye akasema, ‘Paul, kwa nini unajisumbua na hilo?’”

307 Akasema, “Bosi, si—si—siwezi kabisa kuuinua. Ni mkubwa mno. Mzigo huu ni mzito sana kwangu kubeba. Siwezi kuendelea zaidi nao.”

308 Akasema, “Paul, kuna kijito, kinachopitia hapo karibu nawe. Kwa nini usiutupe tu kwenye kijito hicho, kisha uurukie na uendeshe chini kwenye mawimbi? Nacho kinapitia moja kwa moja karibu na kambi.”

Akasema, “Kamwe sikufikiria hilo.”

309 Basi alipoutupa kwenye mawimbi hayo, akaangalia nyuma. Naye Bosi wake alikuwa ni Yesu. Na akasema aliruka tu juu ya hilo gogo, na moja kwa moja akaenda juu ya hayo mawimbi, akiyapiga maji, akipaza sauti, “Nimepanda juu Yake! Nimepanda juu Yake! Nimepanda juu Yake!” Basi kasema alijirudia, naye alikuwa amesimama moja kwa moja katikati ya sakafu, akiirusha mikono yote miwili hewani, akisema, “Nimepanda juu Yake! Nimepanda juu Yake! Nimepanda juu Yake!”

“Sina chochote mkononi ninacholeta. Nimelishikilia tu Neno Lako!”

310 Ndugu, dada, hakuna kitu chema ndani ya mwanadamu yeyote. Hakuna kitu chema katika kitu kingine chochote ila Yesu Kristo. Nami nimepanda juu ya kila ahadi hapa asubuhi ya leo. Na siku moja ninatarajia kupanda niingie Uweponi Mwake juu ya Damu iliyomwagika ya Bwana Yesu Kristo.

Na tuinamishe kichwa chetu.

311 Nimepanda juu Yake. Nimepanda juu Yake. Sio juu ya ushirika wangu, juu ya dhehebu langu, juu ya haki yangu ya kujibunia, bali nimepanda juu ya Neno la Mungu. Ninaamini kwamba, kupitia Damu yenye haki ya Yesu Kristo, siku moja nitamwona Yeye. Nitabadilishwa na kufanywa kama mwili Wake wenyewe wenye utukufu. Nitakuwa katika mfano Wake. Nitamwona Yeye jinsi alivyo.

312 Ninapoiona miaka ikinyemelea, kwangu, maskini nywele zangu nilizo nazo, zikiingia mvi, mabega yangu yakiinama,

sina muda mwingi zaidi. Miaka thelathini na kitu nimekuwa nyuma ya mimbara. Laiti tu ningalikuwa na maisha elfu moja ningeweza kumpa Yeye. Laiti ningalikuwa tu nayo. Ninawapenda watu Wake.

313 Unatumainia kitu gani asubuhi ya leo? Kazi fulani nzuri ambayo umefanya? Kanisa fulani ambalo wewe ni mfuasi wake? Kweli unasimama juu ya Neno la Mungu? Kweli umepata tukio? Umesikia kwamba... Umekuwa na kongamano la kibinafsi na Mungu, na Matokeo yakarudi kama yalivyofanya kwenye siku ya Pentekoste? Si kabadala fulani, si kupeana mikono, ungamo la kimawazo, bali juu ya Moto wa Roho Mtakatifu ukiingia ndani ya maisha yako ambao unabadilisha yote ufanyayo na kusema? Kama hujakuwa na hilo, waweza kuinua mikono yako na useme tu, “Niombee, Ndugu Branham. Mimi si...”? Mungu akubariki. Mungu akubariki. Jamani, huo mkono!

314 Vipi kuhusu nyinyi, Wapentekoste? Baadhi yenu enyi watu, mnaojua, kwamba ki—kidesturi tu mnaenda kanisani, na mnapenda muziki, na nyinyi—nyinyi mnaaweza kutenda kama pentekoste, lakini, kwa hakika, chini kabisa ndani yako, unajua kuna kitu kilichokosekana. Unajua kuna kitu kilichokosekana. Ikiwa kweli unataka, asubuhi ya leo, kwenye meza hii ya kiamshakinywa.

315 Unajua, huenda nisikuone tena kwenye kiamshakinywa kingine, bali ninataka kukuona kwenye Chakula cha Jioni wakati yote yamekwisha. Kamwe hujawahi kuwa na tukio hilo, waweza kuinua mkono wako, useme, “Niombee, Ndugu Branham. Sasa ninataka kuwa...”? Mungu akubariki. Hiyo ni kweli.

316 Unasema, “Hivi kuinua mkono wangu kunafanya chochote?” Kama unamaanisha, kunafanya. Yeye atakuona.

317 Sasa, wewe niamini mimi kuwa ni mtumishi Wake. Watu wengi wameniita nabii. Mimi sidai kuwa nabii. La. Lakini kama unaamini kwamba Mungu hunena na mimi, nisikilize sasa. Kwa uaminifu, unapoinua mkono wako, amini hilo, na uone kinachotendeka kwako. Sasa, kama Yeye ataniruhusu kujua kilicho moyoni mwako, kama Yeye anaweza kuniambia ulichoombea kabla hujaondoka nyumbani, na kile ulichofanya, maneno uliyosema, yale umefanya maishani mwako, na kwamba wewe ulikuwa nani, na mahali unakotoka, na kile kitakachokupata baada ya hapa, na kitendeke, basi hakika Yeye anazungumza na mimi sasa.

318 Hebu tufanye hili kuwa ni kongamano asubuhi ya leo. Vipi kuhusu hilo, enyi Wamethodisti, Wabaptisti, Presbiteri, Wapentekoste, Umoja, Uwili, loo, church of God, Assemblies of God, chochote mlichio? Hebu tuwe tu na kongamano. Hebu tuone kama hatuhitaji upendo kidogo, mmoja kwa mwingine. Hebu tuone kama huo usingeponya jambo hilo kwa namna fulani,

kama tulikuwa tu na upendo kidogo na heshima, zaidi, mmoja kwa mwingine. Mtafanya hilo? Vema.

³¹⁹ Hebu tufanye moja kama Matendo 4, na wewe uungame kila kitu ambacho umefanya ambacho ni kosa. Na papo hapo juu ya meza mahali ulipo, madhabahu hayo ambapo tuliomba baraka, kwenye madhabahu ya familia, hiyo meza ambapo unamshukuru Mungu kwa ajili ya chakula cha kila siku.

³²⁰ Basi, kumbukeni, mnapokula. Kwa sababu mnakula, kitu fulani hakina budi kufa, mpate kuishi, kimwili. Hivi mlijua hilo? Ukila nyama, mnyama alikufa. Ukila mkate, ngano ilikufa. Ukila mboga za majani, mboga zinakufa. Ni namna ya uhai. Na jinsi tu unavyoweza kuishi, kimwili, kitu fulani hakina budi kufa kusudi upate kuishi kimwili.

³²¹ Hilo si ndilo jambo, enyi marafiki, kuwaonyesha kwamba majani ya mtini na mawazo ya kujibunia ya mwanadamu hayatafanya kazi? Ilibidi kitu fulani kife, ili uweze kuishi Milele. Ilibidi kitu fulani kife; si kanisa, si wewe. Ni, ni Kristo, aliyekufa kwa ajili yako. Likubali sasa, utalikubali?

³²² Huku tukiinamisha vichwa vyetu, kila mmoja akiweka moyoni mwako kile unachohitaji. Hata tutakapokutana, Mungu na awabariki.

³²³ Baba wa Mbinguni, nimewashikilia kusanyiko hili la kupendeza la watu. Kwa sababu, sijui mimi. Unajua, huenda huu ukawa ndio wakati wa mwisho. Jambo moja, Wewe unaweza ukaja kabla ya usiku. Unaweza ukaja kabla sijaweza kurudi tena. Lipo jambo moja la hakika: Wewe unakuja. Huenda nikafa. Huenda ikanibidi kuondoka duniani. Wapo wengi hapa ndani. Kama nikija mwaka mmoja leo hii, kuanzia leo, hapana shaka watu hapa ambao hawatakuwapo hapa; wameondoka. Hii ndiyo mara yetu ya mwisho, Bwana, tutakapokutana. Baadhi yetu hapa ndani, tunajua, huu utakuwa ndio mkutano wetu wa mwisho hapa duniani. Wakati mwingine nitakapokutana nao utakuwa kule kwenye Hukumu, nami nitawajibika kwa yale ambayo nimewaambia, kama mhudumu asubuhi ya leo. Nimewaweka kwenye hilo Neno, Baba. Hayo ndiyo yote niyuayo kufanya.

³²⁴ Sasa wapo watu wengi ambao wamesema, katika kongamano hili asubuhi ya leo, wanataka kulizungumzia pamoja na Wewe. Wanafanya hilo sasa, Bwana. Waliinua mikono yao. Wao ni mashahidi kwamba, wao—wao—wao, wao wamechoka, Bwana. Wamechoka. Na wanajua makongamano ya ulimwengu yamekwisha.

³²⁵ Hakuna matumaini tena. Hatuwezi kujenga chochote. Mataifa yote yana mabomu ya atomi, haidrojeni, na ya sumu, na wanaanga, na kila kitu, Bwana. Ulimwengu mzima unatikisika na kutetemeka. Utatakaswa hivi karibuni sana, na kuwa tayari kwa ajili ya ule Utawala mkuu wa Miaka Elfu.

Utatikisika, kama, vipande-vipande. Unapepesuka sasa kama mlevi akiyumba-yumba kwenda nyumbani usiku wa manane, gizani. Hajui anakoelekea.

³²⁶ Ee Baba, bali kuna msingi. Kuna hakikisho, “Kwa kuwa tunapokea Ufalme usioweza kutikisika.” Ninaomba, Baba, ya kwamba kila mmoja ataharakisha aingie kwenye Ufalme huo asubuhi ya leo, katika Kristo Yesu. Wabariki, Baba, walivyoinamisha vichwa vyao, mioyo yao imeinamishwa. Wanangojea jibu sasa. Tuko kwenye kongamano. Tuma jibu sasa hivi, Baba, kwa kila mmoja.

³²⁷ Baadhi yao wanahitaji wokovu. Wengine, mara yao ya kwanza. Wengine ambao ni. . . Nao wata—watasahau tu kanuni zao za imani. Wao, wao wanataka kuipata Hiyo, jinsi ilivyoshuka mara ya kwanza. Wanataka uamuzi Wako. Sio uamuzi wa kanisa, sio uamuzi wa kanuni fulani ya imani; bali uamuzi wa Biblia, uamuzi ambao Mungu alifanya katika Matendo 2, hapo alipomtuma Roho Mtakatifu na Moto juu ya Kanisa. Huo ulikuwa ndio uamuzi Wake, jinsi ambavyo kanisa halina budi kuishi, na kile hawana budi kufanya. Tukiweka kando kila kitu kingine, Baba, tunaungojea uamuzi huo. Ee Bwana, tuma nguvu Zako sasa hivi na umbatize kila mmoja.

Huku tumeinamisha vichwa vyetu:

Walikuwa kwenye chumba cha juu,
Wote walikuwa katika moyo mmoja,
Hapo Roho Mtakatifu aliposhuka
Aliyehidiwa na Bwana wetu.

Hilo ni Neno Lake, ahadi.

Ee Bwana, tuma nguvu Zako sasa hivi,

Ombeni sasa.

Ee Bwana, tuma nguvu Zako sasa hivi;
Ee Bwana, tuma nguvu Zako sasa hivi
Na umbatize kila mmoja.

Ee Bwana, tuma nguvu Zako hivi. . .

³²⁸ Ninaona wahudumu wakiwageuza watu kuelekea mezani, kuomba pamoja nao. Hilo ni sawa.

. . . nguvu hivi. . .

³²⁹ Msifikiri tunasimama tu hapa tukizungumza. Yeye yupo hapa.

Ee Bwana. . .

Kama wewe ni. . . Usimwangelie mtu mwingine. Funga macho yako na umwangelie Yeye, kwa imani.

Umbatize kila mmoja.

Kumbuka:

Walikuwa kwenye chumba cha juu,

Wote walikuwa katika moyo mmoja,
Hapo Roho Mtakatifu aliposhuka
Aliyeahidiwa na Bwana wetu.

330 Sisi hapa, sote kanuni mbalimbali za imani.

Ee Bwana . . .

Tuko katika—tuko katika umoja sasa, sasa. Aminini sasa.

Ee Bwana, tuma nguvu Zako.

331 Angalieni jinsi amekuwa akija kwetu juma hili. Yeye Huyu hapa, papa hapa sasa, papo hapo kando yako, kama utaliadini tu.

Sasa, na umbatize kila mmoja.

Ee Bwana, tuma nguvu Zako sasa hivi,

Ee Bwana, tuma ninii Zako . . .

332 “Ninakupa Wewe moyo wangu, Bwana. Nakupa kila kitu. Huu hapa mkono wangu. Na—najiweka wakfu Kwako sasa hivi. Tuma nguvu Zako juu yangu sasa hivi.

Na umbatize kila mmoja.

Tena:

Ee Bwana . . .

Uimbeni mpaka utakapofanyika halisi kwenu. Mnaona? Sasa funga macho yako, funga moyo wako kwa upumbavu wote na nje kwote.

. . .sasa hivi,

Ee Bwana, tuma nguvu Zako sasa hivi,

Na umbatize kila mmoja.

Ee Bwana, tuma nguvu Zako sasa hivi,

Loo . . .

Ombeni sasa. Mwombeni Yeye Hizo.

. . .nguvu sasa hivi.

Loo . . .

Ungameni makosa yenu.

. . .Bwana, tuma nguvu Zako sasa hivi,

Na umbatize kila mmoja.

333 Sasa, Baba, ninaomba ya kwamba Wewe utausafisha kila moyo. Tunakiri dhambi zetu. Tunakiri makosa yetu. Tumekuwa makosani, Bwana, sisi sote, pamoja. Sote tuna hatia. Tumepungukiwa na utukufu wa Mungu. Ee Mungu, hivi Wewe, katika rehema na huruma, utatwangalia, Bwana? Sisi ni watu wahitaji.

Nasi tunaona ono la Kuja kwa Bwana;

Yeye anakanyaga msimu ambamo zabibu za ghadhabu zimewekwa akiba;

Ameiachilia radi ya majaliwa pamoja na
Upanga Wake mkali sana na mwepesi;
Ukweli Wake, Biblia, inaendelea kusonga
mbele taratibu, kusonga mbele taratibu.

³³⁴ Inasonga mbele taratibu juu ya kanuni za imani. Inasonga mbele taratibu juu ya madhehebu. Inasonga mbele taratibu juu ya kila kitu. Ukweli Wako unaendelea kusonga mbele taratibu.

...tuma nguvu Zako sasa hivi,
Ee Bwana, tuma nguvu Zako sasa hivi;
Ee Bwana, tuma nguvu zako sasa hivi
Na umbatize kila mmoja.

Ee Bwana, tuma nguvu hizo hivi . . .

Ninaliamini, Bwana. Ninaliamini.

Ee Bwana, tuma nguvu Zako sasa hivi;
Ee Bwana, tuma nguvu Zako sasa hivi
Na umbatize kila mmoja.

³³⁵ Wakati muziki ukiendelea, nanyi mnaomba. Sasa, kama ukiusafisha moyo wako kabisa, yote yameungamwa, kweli umeyaweka madhabahuni sasa, sasa Yeye ni Kuhani Mkuu wa maungamo yako. Yeye anaweza tu, anaweza tu kukusaidia kadiri unavyoamini. Kama umezikiri dhambi zako, kama umeyakiri makosa yako, kama umefanya kila kitu, ukakiri umekuwa asiyejali kupita kiasi, chochote ambacho umekiri, sasa yamewekwa kwenye madhabahu ya dhabihu. Sasa weka mikono yako juu ya Yesu na ujitambulishe mwenyewe. Wewe jitambulishe. Kwa imani, weka mikono yako juu ya Yesu. Ndipo basi utakapofanya hivyo, mwangalie Yeye na kusema, "Ninalipokea, Bwana. Ninakuamini Wewe sasa."

Ninaweza, nitaamini, ninaamini;
Ninaweza, nitaamini, nina . . .

Wewe liamini kwa moyo wako wote sasa.

Ninaweza, nitaamini, ninaamini
Kwamba Yesu ananiokoa sasa.

³³⁶ Loo, unaliamini sasa, pamoja na dhabihu yako kwenye madhabahu, juu ya madhabahu? Kile umeweka chini, tofauti zako zote, umeziweka juu ya madhabahu. Sasa, kwa imani, weka mikono yako juu ya Dhabihu yako, Yesu, Ambaye ameketi kwenye mkono wa kuume wa Mungu, kufanya maombezi kwa ajili yako, juu ya maungamo yako, kwamba unaamini kwa moyo wako wote ya kwamba Yeye amekubali kile ambacho umemtolea Yeye. Kama unaamini ya kwamba Yesu Kristo amekubali kile ulichomtolea Yeye asubuhi ya leo! "Nakupa Wewe uhai wangu, Bwana. Nimekuwa baridi. Nimekuwa asiyejali. Mimi, mimi nimefanya mambo nisiyopaswa kufanya. Lakini, tangu saa hii, ninataka kujongea karibu na Wewe. Nami ninaamini ya

kwamba nimeupokea. Ninaiweka mikono yangu juu Yako sasa, ninapofanya maungamo yangu.”

³³⁷ Mnaamini hayo? Unaamini kwamba Mungu alisikia maombi yako? Kama unaamini, mwinulie Mungu mikono yako, useme, “Ninaamini ulisikia maombi yangu. Ninafanya maungamo yangu. Ninaamini Wewe unayasikia maombi yangu. Sasa nitasimama na kukusifu Wewe kwa ajili yake. Nitakupa Wewe shukrani.”

³³⁸ Simameni kwa miguu yenu sasa, na kusema, “Asante, Bwana. Asante, Bwana. Ninakuamini. Sasa ninakupa Wewe sifa kwa kunipa hakikisho hilo moyoni mwangu.”

³³⁹ Sasa inueni tu mikono yenu na kumsifu Mungu, katika njia ya mtindo wa kale, jinsi ambavyo Mungu angewataka mfanye.



63-0608 Makongamano
Ramada Inn
Tucson, Arizona Marekani

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org